# Mnasema Huyu Eti Kuwa Ni Nani?

Phoenix, Arizona, USA
Desemba 27, 1964

1 Habari za asubuhi, marafiki. Hakika ninaona hili kuwa ni majaliwa kuwa hapa katika kanisa hili. Na kwa namna fulani kwanza kabisa ninapenda jina lake. Linaitwa "Jina la Yesu." Ninapenda jambo hilo. Nami na—nafikiri hiyo ni—hiyo ni … Hilo ndilo Jina nililokombolewa kwalo, hilo Jina la kupendeza la Bwana Yesu. Na tena kuwapo ndani hapa pamoja na marafiki zangu, tukiwa tumekusanyika hapa kwenye hii asubuhi nzuri sana ya Jumapili, papa hapa Phoenix. Sijui mahali popote ningependa kuwa, isipokuwa iwe Utukufuni pamoja nanyi nyote. Na hilo ndilo tukio kuu tunalotarajia siku moja.

Nami nilikuwa na wito wa wagonjwa, kuja hapa juu, leo. Nami nilikuwa nikizungumza na Ndugu Outlaw, rafiki yangu mpendwa, naye—yeye alinialika kwa neema sana ku—kuja. Na wahudumu wote hapa Phoenix wamekuwa wazuri sana kwangu.

2 Nashangaa wakati mwingine ni kwa nini nilihamia Tucson. Nimekuwa kule chini miaka mitatu, wala kamwe sijaalikwa kwenye mimbara yoyote. Kwa hiyo nadhani imenibidi … inanibidi tu kufanya ziara yangu ya—yangu hapa Tucson … ama hapa Phoenix, ambako ninajisikia nimekaribishwa. Vema, labda watanizoea … Mwajua, nilihubiri kule chini hivi majuzi usiku, nami nilihubiri saa tatu; si ajabu hawakuniomba nirudi.

Lakini nina—ninajisikia moyoni mwangu kwa ajili ya Mungu na watu Wake. Nami ni mwepesi sana, na ni—ninaogopa nitaacha kitu fulani na nisipate cha kutosha, nami ninaweka jumbe tatu ama nne katika mmoja. Kwa hiyo mimi hakika … kwenu ninyi watu mliokuwa huko chini, naomba msamaha kwa kuwaweka muda mrefu namna hiyo. Haikunipasa kufanya hivyo.

3 Na pia nina furaha asubuhi ya leo kuwa hapa pamoja na Ndugu Carl Williams, na kijana Jimmy hapa, na kwaya, na rafiki yangu ndugu wa Mosley; kumwona Brad, Ndugu John Sharrit, na marafiki zangu wengi sana; Ndugu Pat Tyler, hapa, kutoka huko mbali Kentucky, na—na—na marafiki wengi sana kukusanywa tu katika kusanyiko hili—hili asubuhi ya leo. Mnaona, niliona marafiki wangu wengi kutoka Tucson na kadhalika, wameketi hapa.

Ninafikiria siku moja wakati haya yote yamekwisha, ndipo tutakusanyika mahali ambapo tutaninii … hatuta … ha—hatutalazimika kamwe kuacha kusikiliza muziki huu mzuri, mnaona. Ilitokea tu kwamba niliona ya kwamba mwana wa Ndugu William, ameketi huko nyuma, alitoa ushuhuda usiku wa juzijuzi huko Ramada Inn. Nami nafikiri ana urefu wa karibu futi sita. Lakini nawaambia, baada ya ushuhuda huo, ninaamini alikuwa na urefu wa futi kumi. Yeye alininii tu … Kwa kweli nilithamini yale kijana huyo alisema, ushuhuda mzuri sana.

4 Ninapowasikia vijana hawa wazuri wakishuhudia imani yao iliyo katika Kristo … Nami ni—ninazeeka, na nina-…siku moja sina budi ku—ku—kuondoka na kwenda Nyumbani. Na kuwaona vijana hawa wakija ambao wako tayari, na wakijitayarisha kuendelea kutoka mahali nilipoachia… Na hivyo ndivyo tunavyofanya. Hivyo ndivyo maisha yanavyowekwa. Ili kwamba sisi … kizazi kimoja kitasogea … na baba na mama. Nao wanawalea watoto wao, na kuwaona wakifunga ndoa; na wajukuu wanafuata. Na baada ya kitambo kidogo, Baba na Mama wanaingia mavumbini. Na halafu, ifikapo wakati huo, hao watoto basi wako tayari tena kwa ajili ya wajukuu; na halafu, hao hapo wanaingia ardhini. Lakini kutakuwako na ufufuo mkuu, wa jumla moja ya siku hizi. Sote tutaitwa katika Uwepo wa Mungu kutoa hesabu kwa yale tuliyofanya na yale Mungu aliyotupa: Yesu Kristo. Na kwa hiyo, nina furaha sana kujua ya kwamba nimeishi katika kizazi hiki pamoja na kundi zuri sana la watu, walio ulimwenguni kote, ambao nimekutana nao. Ni—ni—ninamshukuru tu Mungu. Na siku moja wito wangu utakapokuja, vema, itanibidi—itanibidi kwenda kukutana na matendo ambayo nimefanya. Ninawataka wawe wote kwa utukufu na heshima ya Mungu.

5 Kuna mambo mengi ambayo ninapo…tunakaribia Mwaka Mpya ambapo la—laiti ningaliweza—ningaliweza kusahau habari zake, bali ninajua ya kwamba nimeyakiri kama makosa Kwake na—Naye ameyaweka katika Bahari ya Usahaulifu, wala hatayakumbuka kamwe tena. Sasa angalia, hatujaumbwa hivyo, daima tutakumbuka. Tunaweza kusameheana, bali sisi—hatuwezi kusahau jambo hilo kwa sababu sisi—sisi—sisi tumefanywa tofauti. Lakini Mungu anaweza kusamehe na kusahau. Yeye anaweza kulifuta tu kana kwamba halijawahi kutokea. Mnaona? Kwa sababu Yeye ana njia ya kufikia hiyo Bahari ya Usahaulifu, bali sisi hatuna. Hebu wazia tu jambo hilo, ya kwamba Mungu hata hawezi kukumbuka ya kwamba tulipata kutenda dhambi. Wazia jambo hilo! Kwaya, enyi vijana, vipi kama…na hilo je? Mungu hata hakumbuki ya kwamba tulipata kutenda dhambi. Mnaona, Yeye anaweza kusahau jambo hilo lote, na kamwe halitakumbukwa tena. Hilo si lingekuwa ni jambo fulani?

6 Hapa si mahali pa kufanyia mzaha. Siamini katika huko kutania ama kufanya mizaha kwenye… Inanikumbusha juu ya ra—rafiki yangu mmoja. Ameenda Utukufuni sasa. Lakini yeye—yeye alisimulia hadithi ndogo wakati mmoja, juu ya—ya wenzi wa ndoa waliokuwa wamehamia mjini na … kutoka mashambani. Nao walikuwa na ninii … Hawa wanandoa vijana walikuwa na baba mzee, naye alikuwa na moto kweli kweli wa Mungu. Kwa hiyo yule msichana (huyo alikuwa ni baba yake) ninii … kwa hiyo alikuwa amejiunga na watu maarufu sana. Mnajua, ambapo una kila namna hii ya burudani za kisasa. Na kwa

hiyo, alikuwa akitaka kwenda kufanya namna fulani ya burudani siku hiyo nyumbani mwake.

Ndipo—na nanii yake—baba yake, baada ya kula chakula chake cha mchana, hivyo a—angechukua Biblia na kutoka akaingia chumbani na angesoma kwa muda kidogo. Ndipo angeiweka chini, naye angelia, na kupaaza sauti, na kupiga makele, na kuendelea, kisha anasimama na kuvaa miwani yake na kusoma tena. Kisha utafute kitu fulani, na kuweka chini miwani yake na kuanza kulia na kupiga makelele. Huyo mama akasema, "Kelele hizo zingevuruga karamu yangu kwa hiyo i—i—inabidi kuninii…inabidi kufanya jambo fulani na Baba, wala sijui la kufanya." Kwa hiyo akaamua ya kwamba angemwacha aende kwenye orofa ya juu, na apande juu—juu ya ma—mahali pale.

7 Ndi—ndipo akaanza kuwazia, "Vema sasa, siwezi kumpa Biblia yake, maana angefanya jambo lile lile kule juu." Kwa hiyo akampa tu kitabu cha kale cha Jiografia, na kumpeleka kule juu. Kasema, "Baba, angalia picha za kutoka kote ulimwenguni na kadhalika wakati tukifanya karamu." Kisha akasema, "Hatutachukua muda mrefu sana. Tuta—tutakuwa kule chini … Utashuka chini baada ya kitambo kidogo." Kasema, "Ninajua hutaki kukaa mahali palipo na wanawake wote hao."

Akasema, "La, hiyo ni sawa, Mpenzi. Nita—nitapanda kule juu."

Kwa hiyo yeye … Huyo mama alimwashia taa na kumwandalia mahali padogo. Ndipo akawazia, "Vema, hilo—hilo linamaliza shida. Sasa, ataangalia tu picha hizo na kusoma jiografia ki—kidogo, na ndipo…na baada ya kitambo kidogo atashuka aje. Na itakuwa sawa."

8 Kwa hiyo mnamo wakati walipofikia katikati ya kunywa maji yao ya limau la waridi, mnajua, na kufanya karamu yao… Ilikuwa baada ya kitambo kidogo, nyumba ikaanza kutikisika, na mzee huyo akaanza kukimbia huku na huko sakafuni akipiga mayowe na kurukaruka. Na—naye akawazia, "Ni kitu gani kilichompata? Hakuwa na Biblia kule juu. Hiyo … Yeye hana budi alipata Biblia."

Kwa hiyo akakimbia kwenye vipandio, na kusema, "Baba!" Kasema, "Hiyo si Biblia unayosoma. Hiyo ni Jiografia."

Akasema, "Ninajua jambo hilo, Mpenzi. Ninajua jambo hilo! Lakini," kasema, "unajua, hivi majuzi nilikuwa nikisoma katika Biblia ambapo Yesu alisema ya kwamba Yeye aliweka dhambi zetu katika Bahari ya Usahaulifu, unaona, na asingezikumbuka tena. Nami nilikuwa nikisoma hapa ambapo wanasema hata hawawezi kupata kina cha chini kabisa cha bahari kwenye sehemu fulani, katika Jiografia." Kasema, "Wazia tu, wangali wanaenda."

Hilo lilikuwa likimfurahisha. Kwa hiyo unaweza kumpata Mungu po pote utakapoangalia. Mnaona, kama utaangalia tu kila mahali, kila kitu kitamzungumzia.

9 Sasa kwa kweli, kwa kweli, ni—nilimwambia Ndugu Outlaw, "Nitazungumza nini asubuhi ya leo? Umenena ujumbe wako wa Krismasi?"

Kasema, "Naam."

Nikasema, "Ujumbe wako wa Mwaka Mpya?"

"La."

Kwa hiyo, nilikuwa na muhtasari fulani hapa kama nikipata mwaliko mahali fulani, nitazungumza Ujumbe wangu wa Mwaka Mpya. Nilifikiri ningemwachia hilo Ndugu Outlaw kwa ajili yake, juma lijalo.

Kwa hiyo nikafikiri labda ningerejea kwenye somo dogo hapa ambalo huenda likatuweka kwa dakika chache, Bwana akipenda. Nasi tunatumaini ya kwamba Yeye atatubariki. Ninataka kumshukuru Ndugu Outlaw na kanisa hapa, kwa kunialika kuja kuzungumza hapa. Nami … Kama vile Ndugu Outlaw alivyosema, ya kwamba "urafiki wetu kamwe haujapata kunyauka," bali neema ya Mungu imetudumisha miaka yote hii. Hili ndilo kanisa la kwanza lililonialika, nami nilikuja, lilikuwa huko Phoenix.

10 Ninajua … Ninaamini ninamwangalia Ndugu Troll, hapa. Sina hakika … nimeketi mbele. Hiyo ni kweli, Ndugu Troll? Ninaamini alikuwa pamoja wakati huo. Nina vitu vidogo alivyonipa wakati huo; vidogo … wanavifinyanga au kitu fulani. Mnajua, vitu vidogo vya shaba kutoka hapa juu mahali mnapoishi. Nanyi mnaangalia kila mahali … Nami nashangaa itakavyokuwa asubuhi hiyo tutakapovuka, mwajua, na kuwaona watu…wanasema, "Vema, ninii…" Mnajua, tutaonekana tofauti sana wakati huo, kuliko vile tunavyofanya sasa. Tutaninii … Hiyo ni kweli. Hatutakuwa na doa lolote la dhambi wala uzee. Tutakuwa wakamilifu. Loo, ninatamani wakati huo (sivyo?) ambapo shida zote zitakwisha.

11 Na sasa, nina Ujumbe kutoka kwa Mungu ambao na—najisikia. Nami nina … Sitaki kuwa tofauti, bali sina budi kuwa mwaminifu. Na kama sisemi ninayoamini, basi hamwezi kuwa na imani kwangu. Kwa sababu ni—ni—ningekuwa zaidi kama msaliti au mnafiki. Nami ni—ninataka kuwa kitu kingine chochote zaidi ya hicho, mnaona. Huenda nikapoteza marafiki wachache duniani, bali ni—ninataka kukaa mwaminifu kwa imani yangu, kwa yale ninayofikiri ni kweli.

12 Sasa, miaka kadha iliyopita, ilikuwa ni rahisi sana wakati nilipoanza kutoka kwa mara ya kwanza; na zile ishara, na ujumbe, na kuhubiri. Kila mahali mkono ulikuwa umekunjuliwa, "Njoo! Njoo! Njoo! Njoo!" Lakini basi, mnaona, kila ishara halisi kutoka kwa Mungu ina U—Ujumbe, Sauti. Mnaona, inaufuata. Isipoufuata … Mungu hatoi kitu kama hicho kwa ajili tu ya raha ya kukitoa. Yeye—Yeye hutuma kitu fulani kuvutia usikivu wa yale anayotaka kusema. Kama vile tulivyo na uimbaji huu mzuri ambao kwaya hii imefanya; ilikusudiwa kufanya nini? Kuwatuliza watu kwa ajili ya ujumbe unaokuja.

Hivyo ndivyo—hivyo ndivyo ishara inavyofanya. Musa alikuwa na ishara tulizonena usiku uliopita, na ishara hizo zilikuwa na Sauti. Na ninii … wakati ile Sauti iliponena … Yesu alitoka akaenda pia akiwaponya wagonjwa. Yeye alikuwa ni Mtu mashuhuri. Lakini ilipofikia wakati yule—yule Nabii, aliyekuwa duniani … Kwamba hawakuwa na mmoja kwa muda wa miaka mia nne, na huyu hapa alikuwa duniani na akifanya ishara. Ndipo Yeye alikuwa "mtu mzuri," kila mtu alimtaka. Lakini wakati ule Ujumbe ulioifuata hiyo ishara (ile Sauti)…wakati alipoketi chini siku moja, na kusema, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja." Loo, jamani! Hicho—Hicho—Hicho kilikuwa ni kitu cha tofauti. Wao—wao hawakutaka jambo hilo. Mnaona?

Na hilo…ulimwengu uko namna hiyo tu hata hivyo, enyi wapendwa. Mnaona? Wao…chochote wanachoweza kupata, kama wanaweza—wanachoweza kujisaidia nacho, mnaona… Kwamba wao wana—wanajisikia hivyo ilimradi tu haliwasumbui, mbona, wata—watafanya hivyo. Lakini inapofikia wakati ambapo hawana budi kubadilisha mawazo yao kuhusu mambo fulani, hapo ndipo shida inapotokea.

13 Sasa, mnaona, tunajenga jengo, si ukuta. Wajenzi wanataka kuchukua mawe ya kujengea na kushuka kwenda moja kwa moja. Sasa mjenzi yeyote anaweza kujenga hivyo. Lakini inahitaji makanika stadii halisi kupiga kona. Mnaona? Unapoanza kukata kona, huo ndio wakati unaohitajika…inaonyesha iwapo wewe ni—wewe kweli bado ni mwashi ama la; unapoweza kukata kona nao, na kuendeleza mwendeleo huo wa jengo, ukikata kona. Sasa ni kwenye pembe hizi ndipo shida inakuja. Wajenzi wanataka kuendelea kujenga zaidi. Lakini sisi hatujengi ukuta; bali, jengo.

Sasa tunapokaribia jambo hili, asubuhi ya leo, mniombee, nami nita- … Daima ninawaombea. Na sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo katika Uwepo wa Yehova Mkuu, Mungu. Nasi tunatambua upungufu wetu; sote tunatambua. Nasi si mmoja hapa bali tunahitaji. Na sijui, wakati tukiomba, kama kuna mmoja wenu aliye na haja maalum?

14 Mnajua, Mungu asiye na kikomo, kama nilivyosema hapa Phoenix hivi majuzi m—mkutanoni hapa chini… Kama tu televisheni, inakuja, Kristo yuko mumu humu jengoni sasa. Mnaona, kila hatua unayopiga, kila unapopepesa jicho lako, halitakufa kamwe. Iko katika mawimbi ya etha ya hewa. Televisheni haitengenezi hilo. Inachukua tu wimbi hilo lako, na kulileta kwenye skrini. Liko hapo hata hivyo. Ilikuwa hivyo daima. Kila hatua uliyowahi kupiga ingali hai, hewani. Sasa, mnaona tutakavyokuwa kwenye hukumu?

Kwa hiyo, Mungu yuko hapa kwa njia ile ile. Hatumwoni, kama tu vile tusivyoona hizo picha za televisheni. Inahitaji tyubu fulani au kioo cha kitu fulani kuishika sauti hiyo, na kuitoa tena picha hiyo na kadhalika. Hiyo ilikuwa hapa wakati Adamu alipokuwa duniani, bali ndiyo kwanza tu tuipate. Mungu yuko hapa asubuhi ya leo. Na moja ya siku hizi, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, tutatambua. Itakuwa tu dhahiri zaidi kuliko televisheni ama vitu tunavyoviona, ya kwamba Yeye alikuwa hapa mkutanoni asubuhi ya leo.

Sasa wakati sisi … juu ya wazo hilo, weka moyoni mwako kile unachohitaji, na umwinulie tu mkono wako. Utafanya hivyo? Sema, "Bwana, …" Na moyoni mwako, wazia wazo hilo.

15 Sasa, Baba wa Mbinguni, tuna njia hii moja tu, na hiyo ni kwa njia ya maombi. Nasi tuna—tunakuja katika Jina la Bwana Yesu. Ha—hatustahili kulitaja hilo Jina, kulitumia. Sisi hatuninii … kwa vyovyote vile hatufikiri kwamba tunastahili, bali kwa sababu tumealikwa kufanya hivyo. Na akijua jambo hili, ya kwamba Yeye alisema, "Mkimwomba Baba cho chote katika Jina Langu, nita—nita—nitawapa" Nasi tunaninii…laiti tu imani yetu ingaliweza kusimama nyuma ya jambo hilo, kwamba ni Neno Lake na kwamba Yeye ni Nani, ndipo tuna hakika kupata tunayoomba. Umeona kila ombi. Umeuona mkono wangu. Unajua ombi langu.

Na Baba, ninamwombea kila mmoja wao. Kwamba kila kitu wanachohitaji … Bwana, siamini ya kwamba kundi kama hili lingeomba jambo lo lote kwa makosa. Ingekuwa ni kwa ajili ya jambo fulani kwa ajili ya kuendeleza ufalme wao, huenda ikawa ni kwa ajili ya uponyaji wao wenyewe; na kwa kufanya hivyo, wangetaka … ama ufahamu wao wenyewe. Wangetaka hilo kusudi waweze kuuendeleza Ufalme wa Mungu.

16 Nami ninaomba, Mungu, ya kwamba kila ombi la kila mmoja litatekelezwa. Bariki kanisa hili, mchungaji wake, wachungaji wenzi, na mashemasi, wadhamini, washiriki wake wote, waalikwa, wageni. Wao si wageni, Bwana. Sisi sote ni watoto Wako kwa neema na kwa Kristo. Nasi tunaomba ya kwamba utatupa asubuhi hii Mkate wa Uzima sasa, tupate kuondoka hapa tukiwa na ufahamu ya kwamba maombi haya tuliyoomba tumepewa.

Bariki Neno, Bwana, ninapolisoma. Hakuna mtu ambaye—ambaye anaweza ama anatosha kulifasiri Neno hilo. Yohana alikiona kile Kitabu katika mkono wa Yeye aliyeketi juu ya kile Kiti cha Enzi, wala hapakuwa na mtu Mbinguni, wala duniani, wala chini ya nchi ambaye alistahili hata kukiangalia kile Kitabu. Lakini mmoja wa wale wazee akasema, "Tazama, yule—Simba wa Kabila la Yuda ameshinda." Yohana, akiangalia amwone si—simba, alimwona Mwana-Kondoo aliyekuwa amechinjwa, Mwana-Kondoo aliyejaa damu alikuja na kukitwaa hicho Kitabu, akapanda juu ya Kiti cha Enzi na kuketi chini. Nao watu wote mashuhuri wa Mbinguni walitwaa taji zao vichwani mwao na kuinama na kujua Yeye alistahili.

Bwana, tunaomba ya kwamba Yeye atakuja kwenye Kiti cha Enzi cha mioyo yetu asubuhi ya leo. Panda juu na kutwaa kila wazo tulilo nalo, na kuchukua Neno na kunena nasi ili tupate kujua zaidi kumhusu Yeye na mpango Wake maishani mwetu. Tunaomba hili katika Jina la Yesu. Amina.

17 Sasa, kama ukitaka kufungua Biblia kwenye … Maandiko yanapatikana katika Mathayo Mtakatifu sura ya 21, na kuanzia na … Nafikiri tunasoma ninii—kifungu cha 10 na cha 11 cha sura ya 21 ya Mathayo. Kuwa mwema, unapoenda nyumbani, kama hujafanya hivyo katika likizo hizi, kama ungesoma mlango huu wote. Ni mzuri sana. Wote ni mzuri. Huu hasa, kwa ajili ya majira haya, na pamoja na Ujumbe ninaotumaini Roho Mtakatifu atanijalia kuwaletea ninyi asubuhi ya leo.

Angalia aya ya 10 tunaposoma, na ya 11.

*Hata alipoingia Yerusalemu, mji wote ukataharuki, watu wakisema, Ni nani huyu?*

*Makutano wakasema, Huyu ni yule nabii, Yesu, wa Nazareti ya Galilaya.*

Sasa hebu … Mungu aongeze kwenye Neno Lake ma—mazingira ya kusoma Maandiko haya.

18 Sasa tunajua wakati umewadia, na wengi wenu mnajua Maandiko ya sura hii fulani. Ni kwenye … kweli siku ile Kristo alipokuja Yerusalemu, akimpanda huyu punda mdogo. Nasi tunaninii … Kuna hadithi inayosema ya kwamba "alikuwa ni punda mweupe." Ningewazia, katika mfano wa utangulizi wa kuja Kwake mara juu ya farasi wa vita. Wakati huo, nabii alisema, ya kwamba "Yeye angempanda … Mfalme wako anakuja amepanda mwana-punda, na ni mnyenyekevu na mpole." Hivyo ndivyo alivyokuja na—na … juu ya—ya mwana punda, masikini mbeba mizigo. Lakini wakati mwingine atakapokuja kutoka Utukufuni (katika sura ya 19 ya Ufunuo), Yeye anakuja kama Mshindi Mwenye Nguvu. Vazi lake limelowekwa katika damu, akiketi juu ya farasi mweupe, na jeshi lote la Mbinguni linamfuata juu ya farasi weupe. Na hadithi hiyo (si ya Kimaandiko wala ya kihistoria) … Lakini hadithi inaamini ya kwamba Yeye alikuwa amepanda punda mdogo mweupe wakati akiingia Yerusalemu.

19 Sasa hiyo … Nimelichagua hili…bado lingali…kwa sababu tuko katika vivuli vya…ama katika wakati wa msimu wa sikukuu ya Krismasi, na—na wa Mwaka Mpya; kumalizika kwa mwaka uliopita, na mwanzoni mwa mwaka mpya. Siku chache kutoka sasa, watu wengi watakuwa wakifungua kurasa mpya na—na kufanya mambo mapya na kufanya nadhiri mpya; na ni mwanzo wa Mwaka Mpya. Na kwangu kamwe haionekani sana kama Krismasi. Sijui ni kwa nini, daima napenda kuiita "Siku ya Baba Krismasi." Mnaona? Kwa sababu hakuna mengi sana …

Isingekuwa siku ya kuzaliwa kwa Kristo. Kamwe isingewezekana kuwa. Angepaswa azaliwe Marchi ama Aprili, maana Yeye alikuwa ni Mwana-Kondoo. Naye alikuwa mwana-kondoo dume na alizaliwa chini ya kondoo dume, Mapacha. Ilibidi iwe hivyo, mnaona. Na kondoo hawazaliwi Desemba hata hivyo. Kondoo huzaliwa katika majira ya Kuchipua. Na halafu jambo lingine, vilima vya Yuda sasa, kuna futi ishirini za theluji juu yake. Wachungaji wangewezaje kuwa huko nje?

20 Kwa hiyo kweli inatokana na hadithi za kubuni za Kirumi, ambayo ilikuwa ni siku ya kuzaliwa kwa mungu jua. Jua linapopita, siku hurefuka na kuzidi kuwa ndefu, na usiku unakuwa mfupi. Na katikati ya Desemba 20 na 25 ni sikukuu ya kuzaliwa kwa mungu jua, chini ya ninii za Kirumi—hadithi za kufikirika za Kirumi. Na halafu miungu yao … Na ndipo wakaadhimisha siku ya kuzaliwa kwa mungu jua. Naye Konstantino, na—na kuandikwa kwa katiba ya kanisa na taifa na kadhalika. Yeye alisema, "Tutaibadilisha" (bila kujua siku hiyo ilikuwa nini) "na kuiweka kwenye siku ya kuzaliwa kwa mungu jua, na kuifanya: *Siku ya kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu*." Mnaona? Ambayo … Lakini hatujui ilikuwa ni siku gani.

Lakini sasa, yao, wameondoa mengi sana ya Kristo, hata imekuwa ni kila kitu…wengine tena walirudisha hadithi za kiumbe fulani kilichoishi, ilivyodhaniwa, kinachoitwa Mtakatifu Nikolas ama—ama Kriss Kringle, hadithi fulani za Kijerumani. Na yote ni hadithi tu, na Kristo hayumo ndani yake hata kidogo.

Na watu wamegeukia kwenye kununua wiski, na—na kucheza kamari, na mitindo. Na m—mtu ambaye … mfanyabiashara anayeweza kuuza bidhaa zake wakati wa Krismasi anaweza kuishi mwaka mzima, karibu mwaka mzima. Mnaona? Ni likizo kubwa sana, ya kibiashara. Na maskini watoto wadogo mtaani; ambao wazazi wao hawawezi ku—kuwatembelea na za—zawadi, kama ile inayotoka kwa Baba Krismasi, basi wanatembea mtaani, huku maskini mikono yao ni michafu na macho yao ni mekundu. Ni—ninachukia kuona jambo hilo likija. Inapaswa kuwa ni siku yenye uchaji ya kumwabudu Mungu, badala ya kuugua moyo na kuumwa na kichwa na hayo mambo yanayotendeka. Hakuna kitu kwa Kristo juu ya jambo hilo.

Lakini sisi tuko moja kwa moja katikati ya haya yote sasa.

21 Tunajikuta wenyewe, kitu kama walivyokuwa wakati huo. Mnaona, kuingia tu sasa kwenye karamu kuu. Yesu alikuwa akija kwenye Sikukuu ya Pasaka. Naye alikuwa ameingia Yerusalemu … ama akiingia Yerusalemu. Na unabii wa kila kitu alichofanya hauna budi kutimizwa. Kila kitu katika Biblia kina maana. Kila jina lina maana. Hakuna kitu kilichoandikwa katika Maandiko ila kilicho—kilicho na maana kubwa sana.

Nilihubiri hivi majuzi usiku huko Tucson, juu ya *Kwa Nini Ilibidi Iwe Ni Wachungaji Badala Ya Mwanateolojia?* Yeye alizaliwa moja kwa moja upande wa kanisa. Naye Roho Mtakatifu akienda moja kwa moja nyikani na kuchukua, si wanatheolojia, bali wachungaji. Ilibidi iwe hivyo. Wanatheolojia wasingeamini Ujumbe kama huo. Kwa hiyo wao … ilibidi iwe ni wachungaji.

Nilihubiri hapa, miaka michache iliyopita, miaka miwili iliyopita, *Kwa Nini Ilikuwa, Ilikuwa Ni Bethlehemu Mdogo?* Bwana akipenda, Krismasi ijayo, ninataka sisi kuhubiri juu ya, *Kwa Nini Ilibidi Iwe Ni Mamajusi?* Hizi "*Kwa Nini?*"—zina majibu yake, na yako mumu humu katika Biblia.* Nasi tunaishi katika wakati wa ajabu, wakati mkuu sana wa nyakati zote. Tunaishi kufikia kwenye wakati, wakati wowote ambapo utaninii…wakati unaweza kukoma na Umilele unaweza kuchanganyika moja kwa moja pamoja na wakati na kuendelea. Nyakati za manabii wote na wenye hekima, walitazamia. Tunapaswa kuwa macho kila saa, tukikesha kuja Kwake.

22 Tunajikuta wenyewe, kwenye Krismasi hii, kama tu vile walivyofanya Krismasi ya kwanza hata hivyo. Ulimwengu uko karibu kuporomoka. Kama nilivyohubiri wakati mmoja, mahali fulani, kuhusu ujumbe wa Krismasi, *Ulimwengu Unaporomoka*. Na ulimwengu tena uko karibu kuporomoka. Angalia matetemeko ya nchi hapa California. Ninabashiri, kabla ya kuja kwa Bwana Yesu, ya kwamba Mungu atapazamisha mahali hapo. Ninaamini ya kwamba Hollywood na Los Angeles, na sehemu hizo chafu kule, ya kwamba Mungu Mwenyezi atazizamisha. Yataenda chini ya kilindi cha bahari. Na kuna dhambi nyingi sana, unaona, ni kile kizuizi.

Ustaarabu umesafiri pamoja na jua, kutoka … na ulianza Mashariki, ukielekea magharibi. Na sasa uko kwenye Pwani ya Magharibi. Kama ukienda mbali zaidi, utarudi Mashariki tena. Kwa hiyo hicho ndicho kizuizi. Nayo dhambi imesafiri pamoja na ustaarabu, na umekuwa ni shimo la maji machafu ya nyakati zote. Mambo wanayofanya ambayo—ambayo wanadamu katika wakati mwingine wowote wasingeweza kuwazia jambo kama hilo. Wanawake wamejitupa kwenye takataka nyingi sana, hata hakuna mwanamke katika wakati wowote angaliweza kufikiria jambo kama tunalofanya siku hizi. Na halafu bado tunajiita Wakristo. Ni aibu iliyoje!

23 Si ajabu yule nabii mkuu akainuka, naye akasema, "Mimi si nabii wala mwana wa nabii, bali …" Kasema:

> *Simba amekwisha kunguruma, basi ni nani asiyeweza kuogopa? Na…Mungu amenena, basi ni nani anaweza kujizuia kutabiri?*

Mnaona? Kuna kitu ambacho hakina budi kupaza sauti.

Tuko katika saa ya hatari sana; ulimwengu uko hivyo. Lakini Kanisa, Kanisa halisi (si madhehebu); bali Kanisa, Lenyewe, liko tayari kwa ajili ya ushindi mkubwa sana liliopata kupata: kule kuja kwa Bwana Arusi kwa Bibi-arusi.

Tunatengana, tukimtazamia masihi fulani (kitu fulani) aje na kutuokoa, kututoa katika hayo yote. Tunaangalia chini…mizozo kule Mashariki. Tunaangalia huko Afrika kwenye maasi, na shida za ubaguzi wa rangi, na kuchanganyikana, na—na ubaguzi. Nasi sote tulizozana na kupaaza sauti hapa si muda mrefu sana uliopita (marafiki zetu weusi) kuhusu, "Lazima tuninii, lazima tuchanganyikane. Hicho ndicho tunachohitaji. Hatuna budi kuwa na ushirikiano; kila mtu, sawa, kila mtu." Vema, hilo ni sawa kabisa. Hilo ni sawa kabisa. Siamini katika utumwa. Kwanza hao watu hawakuwa ni watumwa. Wao si watumwa.

24 Mungu ni mbaguzi. Mimi pia. Mkristo ye yote ni ubaguzi. Mungu huwatenganisha watu Wake na hao wengine wote. Wao ni … Daima kumekuwapo na ubaguzi. Yeye alichagua taifa. Yeye huchagua watu. Yeye ni mbaguzi. Yeye aliumba mataifa yote. Lakini hata hivyo, Mkristo halisi wa kweli hana budi kuwa mbaguzi. Akijitenga na mambo ya ulimwengu na kila kitu, na akaja katika kusudi moja, Yesu Kristo.

Lakini wao wanapigia kelele jambo hilo. Nimejaribu kuwaambia, "Hicho si kitu kitakacholiokoa taifa letu. Huo ni mpango wa kisiasa tu. Ni ja—jambo lenye msingi wa kikomunisti." Nafikiri Martin Luther King atawaongoza watu wake kwenye mauaji makubwa sana, na mauaji ya kinyama, waliyopata kuwa nayo. Nao … Mnaona, hilo halitauunganisha ulimwengu pamoja. Hilo halitatuokoa. Tumewapa kuchanganyikana. Sasa hali ni mbaya sana kuliko ilivyowahi kuwa. Mnaona, hilo si ninii … hilo silo swali. Kuna kitu kimoja tu kinachoweza: hicho ni Mungu. Nao hakika hawalitaki.

Hawakumtaka wakati huo. Walikuwa wanasambaratika, na siasa zao zilikuwa zikivunjika, mataifa yao yalikuwa yakivunjika, makanisa yao yalikuwa yakivunjika, nao walikuwa wakilia wampate Masihi fulani.

Walimtaka. "Loo, tutumie Masihi." Lakini wakati alipokuja …

25 Mungu alitoa … anajibu jibu la maombi yako. Umeomba, nawe utapokea. Na hiyo ni … Ningeweza kusimama hapa kwa saa nyingi, juu ya wanaume na wanawake, Wakristo hata, kuomba kwa ajili ya kitu fulani; na Mungu hutoa jibu na hata hawalitambui.

Na sasa, Mungu aliwapa jibu. Wao wanataka Masihi. Walijua ya kwamba walikwisha kuwa na Makaisari, nao walikwisha kuwa—walikwisha kuwa na akina Daudi, walikwisha kuwa na akina Sulemani (yule mtu mwenye hekima), walikuwa na akina Daudi (mashujaa wakuu wa vita), wao—walikwisha kuwa na kila namna, bali walijua iliwabidi kupata msaada kutoka Mbinguni nao… Mungu alikuwa amewaahidi Masihi. Naye akawatumia huyo Masihi, katika jibu la maombi yao, bali hawakumtaka.

26 Nashangaa, leo, kama maombi yetu … Unawasikia wakisema, "Ombeni kwa ajili ya ufufuo mkuu. Omba kwa ajili ya jambo *hili*. Ombeni kwa ajili ya ushindi. Ombeni kwa ajili ya umoja." Nashangaa, kama Mungu angetuma mpango kama huo, kama tungaliukubali. Nashangaa tu kama tungekubali yale anayotutumia. Mnaona, Yeye … Sababu ya sisi kuombea vitu hivi, ni kwa sababu tunajua vinahitajika. Lakini wakati Mungu anapolituma jinsi anavyotaka, basi si kulingana na ladha yetu, na kwa hiyo hatutalipokea. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa katika siku hiyo. Kama Yeye hakuwa katika ladha ya imani yao na … Wao—wao wasingempokea tena, leo. Hiyo ndiyo sababu waliuliza swali hili, "Ni nani huyu? Jamaa huyu anayekuja ni nani?" Mnaona, ulikuwa ni wakati—mzuri sana. Loo, kila mtu alikuwa … wasiwasi. Kitu fulani kilikuwa karibu kutukia.

27 Na hebu uangalie ulimwengu leo, ni wasiwasi wa namna gani ulimwengu mzima unaoishi nao. Unashuka kwenda barabarani … Hata—si salama kuendesha gari. Si salama kuwa katika barabara kuu yenye njia nne. Kila mtu yuko kwenye wasiwasi, anapiga kelele na … Kuna nini? Tulia. Unaenda wapi? Hilo ndilo linalofanya hospitali za wenda wazimu kujaa. Hilo ndilo limeliletea kanisa machafuko kama hayo. Wao wana—wana kichwa kigumu sana juu ya jambo fulani. Hawatasimama na kutafakari Neno la Mungu, na saa tunayoishi; wote wamelemewa na uchovu, wasiwasi.

28 Na sasa, tunajua. Tunafahamu. Dunia ndiyo kwanza ipitie maumivu makali sana ya kuzaa. Na kanisa linapitia katika utungu wa kuzaa. Ilibidi lipitie utungu wa kuzaa kabla ya kutoa … Kila mmoja wa manabii, walipokuja ulimwenguni, ilikuwa ni uchungu wa kuzaa kwa kanisa. Ulimwengu umepitia kwenye Vita vya Kwanza vya Dunia, Vita vya Pili vya Dunia, na sasa uko tayari kwa Vita vya Tatu vya Dunia. Na iko katika utungu wa kuzaa tena. Lakini kuna kitu kimoja tu kinachoweza kuleta amani, na hicho ni Kristo.

Mifumo yetu yote, na mawazo yetu, na makanisa yetu yanajenga, na siasa zetu zote, na sayansi yetu yote na kila kitu, imethibitishwa ya kwamba ni upuuzi. Na halafu tunamwomba Mungu a—atusaidie, aingilie kati, "Njoo utufanyie jambo fulani." Na basi anapofanya jambo hilo, sijui kama tungeweza kufahamu jambo Hilo; kama tungeweza kulipokea; ama hata tungaliweza kulifikiria?

29 Sasa hilo ndilo lililofanywa huko nyuma katika siku hizo. Walikuwa wakiomba, waliisha kuwa na kila namna ya viongozi wakuu, waliishakuwa chini ya serikali mbalimbali, waliishakuwa chini ya ufalme, waliishakuwa chini ya kila kitu, waamuzi. Lakini walijua ya kwamba kuna kitu kimoja tu ambacho kingeweza kuwaokoa, hicho kilikuwa ni kuja kwa Masihi. Na *Masihi* maana yake ni "aliyetiwa mafuta." Mwanadamu aliyetiwa mafuta. Ndipo mwanadamu, aliyetiwa mafuta na Neno. Neno lililofanyika mwili miongoni mwetu. Na wakati alipokuja, ha—hakuwa na ladha ya jinsi vile walivyomtaka hasa awe; si ladha waliyokuwa nayo…ambayo anapaswa kuja nayo. Kwa hiyo basi wao—wao—wao wanalia, "Ni nani jamaa huyu? Ghasia yote hii ni ya nini?" Kundi la wakulima wadogo pale langoni, wakivunja mitende na…

Naye akasema, "Mbona, hebu wanyamazishe. Wanatukera, jinsi wanavyoshangilia, na kupiga vifijo, na kufanya ghasia."

Yeye akasema, "Wakinyamaza, miamba hii mara moja itapaza sauti."

30 Loo, wakati ulikuwa ukifunuliwa! Unabii ulikuwa ukitimizwa. Si ajabu! "Simba ananguruma, ni nani hatahofu? Na Mungu amenena. Ni nani atakayejizuia kutabiri?"

"La, kama hakuwa katika ladha yetu wenyewe hasa… Kama asingalikuwa jinsi tu tulivyomtaka, jinsi ambavyo tulidhani angalipaswa kuja, tusingalimpokea." Basi, kanuni zao za imani ndizo zilizowatoa kwenye Neno lililoandikwa. Walikuwa wameliacha kwa mbali sana, walishindwa kumtambua Yeye waliyekuwa wameomba aje. Makanisa yao yalikuwa yamewapeleka mbali sana, mpaka jambo lile lile walilokuwa wameliomba, lilikuwa papo hapo pamoja nao, na halikuwa katika ladha yao, na kwa hiyo wao—wao—hawakuweza kuliamini. Ilibidi wajiepushe Nalo. Ilibidi wajiepushe Nalo. Walilitupilia mbali. Wao … Kuna jambo moja tu unaloweza kufanya wakati unapokutana na Kristo. Hiyo ni ama kumkubali Yeye ama kumkataa. Huwezi kuondoka ukiwa pande zote mbili. Huwezi kufanya hivyo. Si—si kazi yako kufanya hivyo. Ni hivyo tu.

31 Hebu angalia tu, jinsi wachache walivyomtambua kuwa Neno Lililotiwa Mafuta, la siku ile. Mnaona, Mungu hapo mwanzo, akiwa asiye na kikomo, na aliyejua mambo yote tangu mwanzo… Na jambo pekee

ambapo vitu hivi vilivyo ni kwamba ni onyesho la sifa Zake. Sifa … Una sifa. Ni wazo lako. *Unawazia* jambo fulani, kisha unalinena, halafu unalichukua. Huyo ni Mungu. Yeye, hapo mwanzo … Kama wewe ni … Kama uliwahi kuwa au utapata kuwa Mbinguni, hapo mwanzo ulikuwa Mbinguni. Wewe ni sehemu ya Mungu. Wewe ulikuwa wazo Lake. Yeye alijua jina lako. Yeye alijua wewe ulikuwa nani kabla hakujapata kuwa na m—m—molekuli, kabla hakujakuwako na nuru. Kabla hakujakuwako na cho chote, Yeye alikujua wewe na jina lako. Na kuliweka kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kabla ulimwengu haujapata kuumbwa. Mnaona, wewe ulikuwa ni wazo Lake. Na halafu ninii … Ndipo unakuwa Neno. Na neno ni—ni wazo lililotamkwa. Ndipo unadhihirishwa.

32 Hivyo ndivyo alivyokuwa. Hapo mwanzo alikuwa peke Yake. Mungu aliishi peke yake na mawazo Yake. Kamwe hatafanya hivyo tena maana mawazo Yake yanadhihirishwa. Na hiyo ndiyo sababu tuko papa hapa, siku hii … ni Mungu akishirikiana na mawazo Yake, akidhihirishwa. Mnaona? Tuko hapo. Kwa hiyo, wewe, kwa kuwazia, huwezi kuongeza mkono mmoja kwenye kimo chako. Huwezi kufanya *hivi, vile*, ama *vinginevyo.* Ni Mungu anayeonyesha rehema. Ni Mungu. "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, wala hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu." Hilo latosha.

33 Sasa, hebu angalia, jinsi ambavyo wachache wao katika siku Zake, kati ya mamilioni juu ya nchi, ambao hata hawakujua kitu juu ya Yeye kuwapo hapa. Hebu wazia tu, kulikuwako na makumi … mamilioni ya watu ambao hawakujua kitu juu yake. Na kuwazia, katika Israeli wakati huo, kulikuwa na watu milioni mbili na nusu huko Palestina, ya Waisraeli, wala hakuna mmoja kati ya mia moja waliowahi kujua hilo. Si ajabu Yeye alisema, "Mlango ni mwembamba na njia imesonga, bali ni wachache watakaoiona." Hebu wazia tu ni wangapi hawakumtambua! Sikujua ya kwamba Yeye alikuwa Ndiye. Na wao walikuwa moja kwa moja karibu na mahali alipokuwa Yeye; hiyo ndiyo sehemu inayohuzunisha.

Wale waliotembea pamoja Naye, na kumwona huko mtaani, na kadhalika…wao—wao hawakutambua kwamba Yeye alikuwa ni Nani, kwa maana Shetani alihakikisha ya kwamba Yeye alikuwa na ji—jina chafu kupindukia ambalo mtu angeweza kupewa. Yeye aliitwa na ulimwengu (ulimwengu wa kawaida)…A—aliitwa mwana haramu (kwa sababu alisema ya kwamba "mama yake, aliyekuwa amzae Yeye, kwa Yusufu, kabla hajaolewa naye"). Kwa hiyo akampa jina haramu.

34 Na tena, ka—kanisa lilimwona katika nguvu Zake kuu za kudhihirisha. Akidhihirisha nini? Si kudhihirisha kanuni ya imani! Alikuwa akidhihirisha Neno! Yeye alikuwa Neno lililotiwa Mafuta, Mwenyewe. Nao walipoona jambo hilo likitukia (kule kudhihirishwa, yule Masihi aliyetiwa mafuta), walimkataa. Hawakumtaka. Hakuwa katika ladha yao. Hiyo ndiyo sehemu ya kusikitisha. Ni wangapi …? Wazia tu jambo hilo! Kama tu katika siku zingine.

Mnaona, kila mmoja alikuwa na fasiri yake ya Neno. Hiyo ndiyo sababu … sababu ya Israeli kutomtambua Musa. Hiyo ndiyo sababu ulimwengu haukumtambua Nuhu. Hiyo ndiyo sababu manabii wote hawakutambuliwa. Wana tafsiri yao wenyewe ya Neno. Lakini Mungu, katika kila wakati, amekuwa na Masihi Wake. Mnaona? Kuukataa Ujumbe wa Nuhu, ilikuwa ni kumkataa Mungu. Kumkataa Nuhu, ilikuwa ni kuangamia. Kumkataa Musa, ilikuwa ni kuangamia. Ilikuwa … Walikuwa ndio Masihi Watiwa Mafuta wa wakati huo, Neno lililoahidiwa kwa ajili ya wakati huo. Na wakati Yesu alipokuja, Yeye alikuwa utimilifu wa Neno.

Mungu, Mwenyewe, alifanyika katika umbo la mwanadamu, akiwa na mifupa na nyama; Mtiwa Mafuta. Nao walipaswa kuona jambo hilo. Lakini mnaona, ninii yao—ulimwengu wao wa kanisa ulikuwa umeongeza sana hapa na kuondoa hapa na—na kadhalika, mpaka lilikuwa limechafuliwa sana mpaka wa—waliliamini kanisa lao badala ya—ya Neno. Ndipo wakati walipoona kanisa lao limetiwa mafuta, ndipo walidhani jambo fulani kuu lilikuwa likitendeka. Lakini walipoona Ne—Neno limetiwa mafuta, ndipo wakasema, "Huo ni ushupavu wa dini. Mtu huyu ni ibilisi, Beelzebuli." Maana lilikuwa ni jambo lililo kinyume sana na kanisa lao mpaka…kanuni zao za imani ya kanisa na yale waliyokuwa wamefanya. Na ilikuwa hivyo katika kila kuja kwa nabii, kanisa lingekuwa limechafuka sana.

35 Mungu alituma sheria Zake na kuwapa agano. Naye kuhani angekuja na kukata, na kuongeza kwenye hayo, na kupeleka hapa, na kufanya kanuni ya imani kutokana nalo. Halafu basi, Mungu angeinua kutoka mahali pasipojulikana, mtu fulani aliyetiwa mafuta aliyekuzwa katika nguvu za Roho. Naye daima alichukiwa na makuhani, na wafalme. Na—na ambapo manabii wa uongo walivaa mavazi yao mororo, na kutembea kwa unyenyekevu, na kwa upole miongoni mwa wafalme na makuhani, ili wastahili majina makubwa na—na kadhalika. Ndipo nabii halisi na wa kweli, alikuja kutoka mahali pasipojulikana, si katika madhehebu yao yoyote.

Je! ku—kumewahi kuwako na mahali popote katika Biblia, ambapo Mungu aliwahi kumchukua kuhani na kumfanya nabii? Ni wapi ambapo Mungu aliwahi kumchukua mwanathiolojia wa kikanisa (mtu aliyefunzwa, mwanathiolojia aliyefunzwa) na kumfanya nabii? Hakuna kamwe katika historia za mahali popote, ambapo Yeye aliwahi kufanya jambo hilo, katika wakati wowote…Yeye alipopata kufanya hivyo. Yeye hana budi kuondoka kutoka katika mfumo huo, na kumleta. Na hivyo ndivyo alivyokuwa amefanya hapa.

36 Yesu, alipozaliwa katika Bethlehemu ya Yuda, kutoka katika familia maskini, naye hawakuwa na historia ya alikotoka kadiri walivyojua, ni kabila moja tu la—la Yuda, na mama Yake na baba yake walikuwa wanatoka katika ukoo wa Daudi; nao iliwabidi waje wakatozwe kodi. Naye huyu hapa, jamaa mdogo tu, kila mahali … hafanyi lolote ila kuyararua makanisa. Nao walimchukia. Wala wasingeweza kusema lolote ila kwamba mtu huyo alifanya miujiza. Petro alielezea hayo kwenye Siku ya Pentekoste, alisema, "Yesu, wa Nazareti, Mtu aliyethibitishwa na Mungu miongoni mwetu, ya kwamba Mungu alikuwa pamoja Naye." Na si kuongezea kwenye Neno Lake ama chochote kile; ili kulifanya dhahiri zaidi: "Alikuwa ni Mungu aliyefanyika mwili pamoja nasi. Mungu pamoja nasi." Mungu pamoja nasi."

37 Na kusema hivi majuzi usiku, ya kwamba Musa, akisimama pale na mkono wake kifuani mwake, yeye … huyo alikuwa ni Mungu katika Musa. Yeye…(akishika siri moyoni mwake), naye akaunyosha ukiwa mweupe kwa ukoma. Kisha akaurudisha tena kifuani mwake na kuuponya, halafu tena akaunyoosha tena kwetu wakati alipomtuma Roho Mtakatifu; ambaye alikuwa ni Mungu, tena, katika umbo lingine tu katika Siku ya Pentekoste. Nasi tunamkataa. Hatumtaki Hiyo. Hivyo ndivyo walivyofanya wakati huo. Hivyo ndivyo ambavyo labda tungefanya leo.

38 Tunaona, kila mtu ana tafsiri yake mwenyewe. Hiyo ndiyo sababu linatatiza sana. Lakini unajua, Biblia ilisema, ya kwamba, "Neno hili si la kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani." Halihitaji fasiri ya Kipresbiteri. Halihitaji fasiri ya Kibaptisti. Wala halihitaji fasiri ya Kipentekoste. Mungu ndiye anayejifasiria Mwenyewe. Yeye alisema atafanya jambo hilo, kwa hiyo Yeye analifanya tu, na hilo latosha. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu wanaliona Neno la ahadi lililotiwa mafuta na ndipo wao—hawawezi kulipokea. Mnaona, kwa sababu ni kinyume cha kanuni za—zao.

39 Jinsi Masihi (Mtiwa Mafuta) angeonekana, na yale angefanya; ilikuwa mbali na ufahamu wao. Na ndipo waliposomewa kutoka katika Maandiko, yale atakayofanya, bado hawakuelewa. Kwa kuwa wakati hawa mamajusi waliposhuka wakaja, kutoka huko Babeli, kwa namna fulani walikuwa kaskazini-mashariki kutoka Yerusalemu, na wakaangalia chini na kuiona ile Nyota ikiongoza kuelekea magharibi. Waliifuata kwa muda wa miaka miwili, wakishuka kuvuka Mto Tigris, na kupitia katika mabonde ya Shinari, na wakashuka wakaja, wakafikia kwenye mji mkuu wa dini zote. Dini iliyo kubwa zaidi ulimwenguni, katika hekalu, huko Yerusalemu. Nao wakaenda huku na huko mitaani wakisema, "Yuko wapi? Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?" Mbona, hakuna mtu aliyejua kitu juu yake. Ilikuwa ni ajabu.

40 Hata liliwashtua Baraza la Wazee…likaita wasomi na kusema, "Someni katika Maandiko ambapo Masihi…"

Nao wakaenda na kuyachukua Ma—Maandiko na kusoma ya kwamba Mikaya alisema, ya kwamba "Kutoka…Yuda…Bethlehemu ya Yuda, wewe hu mdogo sana katika majumbe wote? Lakini katika wewe atatoka mtawala huyu."

Mnaona, badala ya kuchunguza, walilipuuzia tu, "Vema, ni lundo la ushupavu wa dini." Mnaona? Hiyo ndiyo sababu wachungaji waliuchukua Ujumbe. Mnaona, hawaninii … Wana tafsiri yao wenyewe, kwa hiyo, wao—wao wanakosa jambo halisi lililo kweli.

41 Lakini kama ilivyokuwa, alipokuja, Yeye alikuja jinsi hasa Neno lilivyosema angekuja. Aliingia mjini vile vile hasa, katika somo letu asubuhi ya leo, jinsi Neno lilivyosema Yeye angekuja. Nao wakasema, "Ni nani huyu?" Mnaona ninalomaanisha? Walipaswa kujua ilikuwa ni nani. Na hapa … si ulimwengu wa nje, bali ulimwengu wa kanisa ulisema, "Ni nani huyu? Ni nani huyu?" Wakati, pale, Maandiko yalikuwa yamesema dhahiri ya kwamba hivyo ndivyo hasa angekuja. Nao wanasema, "Huyu ni nani? Jamaa huyu ni nani? Mhemko huu wote unahusu nini? Acha kufanya makelele hayo yote. Inatufanya tuwe na wasiwasi." A-ha. Mnaona? Ninii … Mnaona? Kitu kile kile walichokuwa wameomba kilikuwa papo hapo mikononi mwao, nao hawakumtambua. Naye alikuja jinsi hasa Maandiko yalivyosema angekuja. Na kama akija leo, Yeye atakuja jinsi Maandiko yasemavyo Yeye atakuja. Yeye daima huja katika ladha ya Neno la Mungu, na si kwa ladha ya wazo la mwanatheolojia fulani kuhusu hilo.

42 Jambo lingine, je! Ulijua Neno la Mungu kamwe halikumjia mwanatheolojia? Tafuta Maandiko ambapo lilipata kumjia. Neno haliji kwa wanatheolojia; hata kidogo. Lakini mnaona, kama Neno lilidhihirishwa leo, Neno la siku yetu, lingekuwa katika ladha ya Neno la Mungu. Si kwa ladha ya wazo la mtu fulani. Mungu angechukua Neno Lake aliloahidi kwa ajili ya siku hii, na kulitia mafuta, na lingetukia. Hivyo tu. Hakuna njia ya kulizuia litukie. Litafanya hivyo haidhuru, haidhuru kanisa linasema nini na hao wengine wanaamini nini. Ni … Mungu atafanya jambo hilo hata hivyo. Kutakuwako na wachache sana watakaopata kujua habari zake. Hiyo ni kweli, wachache tu. Daima imekuwa hivyo.

43 Mnaona, kwa fasiri yao wenyewe, wasingeweza kufanya jambo lingine kwa maana waliegemea kwenye yale kanisa liliyowaambia. Lakini Yeye angekuja…Daima Yeye huja wakati huo…Alikuja wakati huo, hasa, na angefanya hivyo kila wakati anapokuja, na kila kitu anachofanya, kitakuwa katika ladha ya Neno. Kwa hiyo basi, hatuwezi kutumaini yale watu wengine wanasema. Kuna kitu kimoja tu unachoweza kutumaini, na hicho ni Neno. Nalo Neno ni Mungu. Na Neno linapotiwa mafuta humfanya Masihi; Neno lililotiwa mafuta la wakati huu. Ni zuri iliyoje! Wao walilikosa, hilo Neno; ile kweli… Walikuwa na … Neno

daima ni kweli, bali tafsiri yao juu Yake ilikuwa ni makosa.

44 Sijui kama kitu hiki kikubwa, Baraza hili la Ekumeni tulilo nalo ulimwenguni siku hizi, na Baraza la Makanisa Ulimwenguni linalojiunga pamoja kutufanya sisi sote kitu kimoja… Sijui kama wanatambua kama … Hilo ndilo hasa Maandiko yalisema wangefanya. Lakini wao wanafikiri ndilo jambo la ajabu sana ulimwenguni, kwamba sisi sote tunaweza kushikana mikono na kuwa mmoja. Kasema, "Yesu aliomba kwamba sisi tupate kuwa mmoja." Hiyo ni kweli. Lakini si mtu wa namna hiyo.

Yeye alisema, "Mwe mmoja kama Mimi na Baba Yangu tulivyo mmoja." Naam, uwe mtu wa namna hiyo. Basi hilo litakuwaje? Neno ndani yetu lingekuwa ni Neno lililotiwa mafuta. Huo ni umoja wa Mungu. Mnaona, umoja wa Mungu ni Neno lililotiwa mafuta ndani yako. Mnaona? Na halafu unakuwa mwana (masihi) wa wakati huu.

45 Sasa tunawaona watu vivyo hivyo. Watu hawabadiliki. Watu hawa waligawanyika katika makundi matatu. Nasi tutaangalia jambo hilo kwa dakika chache sasa. Ninajua nitachelewa kidogo tu, kama ni sawa kwenu. Mimi ni mwepesi sana, ni—ni—ninaninii tu … Sijui; ni—ninaingia na kuandika Maandiko, na mihitasari midogo. Na ndipo ni—ninafika pale na Ro—Roho Mtakatifu ananyakua moja, nami ni—ni—ni—ni… inaonekana tu kana kwamba hakuna mwisho wake. Linaendelea tu. Lakini, sasa, kwa somo letu.

46 Walikuwa wamegawanyika, pale, katika makundi matatu mbalimbali, wakiwa na maoni matatu mbalimbali. Baadhi yao walimwamini. Baadhi yao walimchukia. Na baadhi yao hawakujua la kufanya.

Mnaona? Hivyo—hivyo ndivyo tu tulivyo nalo. Nilihubiri, ninaamini katika kanisa hili, wakati mmoja: *Waaminio, Wanaojifanya Waaminio*, na *Wasioamini*. Hao watatu katika kundi, u—una hao kila mahali. Hawa ni watatu katika kundi, pia; kwa kuwa hii ndiyo hali watu wamekuwa nayo daima. Tunaweza kurudi nyuma kabisa na kuthibitisha, hiyo ndiyo hali ya watu daima. Daima wamekuwa katika hali ya namna hiyo.

Tena kwa kuwa daima imekuwa namna hiyo, basi linatufanya kuelekea kuamini ya kwamba Mungu aliwaumba watu wawe namna hiyo. Mbona, Yeye atamfanya adui Wake kumsifu. Kila kitu … Paulo, akiandika, katika Warumi, sura ya 8, alisema, "Loo, ewe mpumbavu. Je! udongo u—unaweza kumwambia mfinyanzi, kwa nini kufanya ninii yangu…kunifinyanga hivi? Je, Yeye hana mamlaka ya kukifanya chombo kimoja cha heshima na kingine kisicho na heshima?" Vipi kama Yeye hakuwa ameumba usiku? Huwezi kamwe kufurahia mwangaza wa jua. Kama wakati wote ungalikuwa ni mwanga wa jua, usingejua jinsi ya kuufurahia. Vipi kama kusingekuwako na maradhi? Usingejua jinsi ya kuithamini afya njema. Vipi kama kusingekuwako na watu waovu? Hakuna wanawake waovu? Mwanamke mzuri asingeheshimiwa. Mnaona? Wasinge … Heshima isingalikuwa yake, maana wote wako hivyo tu, ni kitu kimoja tu kinachochosha. Lakini ni sheria ya tofauti.

47 Mungu hufanya namna hiyo: mmoja wa kufedhehesha sana, apate kumwonyesha mwenye kuheshimika; mmoja kuwa aliyekosea sana, inaonesha… Kama haikuwa hivyo, hilo lingekuwa jambo sahihi. Kama hakukuwa na … Hakuwezi kuweko na dola ya bandia mpaka kuwe na dola halisi. Na halafu bandia ni … Kama kwanza ingalifanywa tu ya bandia, basi ingekuwa ndiyo iliyo halisi. Lakini ni—ni nakala. Hakuwezi kuweko … Hakuwezi kuwa na dhambi mpaka kuwe na haki. Kwa sababu haki ni ninii—kitu sahihi, na dhambi ni upotovu wa haki. Kwa maneno mengine, ukweli ni ukweli. Uongo hauwezi kuwa uongo mpaka kuwe na ukweli kwanza; kuupotosha ukweli huo kuwa uongo. Kwa hiyo dhambi yote si kitu ila haki iliyopotoshwa. Kwa hiyo, kuna mfumo ulimwenguni.

48 Mifumo miwili; na mmoja wao ni mfumo sahihi, na huo mwingine ni mfumo uliopotoshwa. Na moja ya hayo ni Neno la Mungu, ambalo ni kweli; na kila neno la mwanadamu ni uongo. Na mfumo huu wa kimadhehebu tulio nao siku hizi, wanaounda Baraza la Makanisa Ulimwenguni kufanya alama ya mnyama kuwaunganisha pamoja, ni jambo baya. Na wanadamu wanaingia ndani yake kwa upofu.

Mungu tayari ameweka kitu duniani cha kuwakomboa. Lakini wao wanafikiri ni kundi la ushupavu wa dini. Hawakitaki. Wanakikataa. Wanafikiri hawana budi kufanya jambo fulani juu ya jambo hilo. Hawana budi kutengeneza mfumo wao wenyewe. Mungu ana mfumo tayari hapa, Neno Lake. Bali hatutaki Hilo. Kwa hiyo tunajikuta leo, kama tu walivyokuwa wakati huo.

49 Na sasa, tukiona ya kwamba watu wamekusudiwa kuwa hivyo … Angalia, unasema … Ninajua ninachukua muda mwingi, bali sitaki kuendelea kuangalia hilo kwa sababu linanifanya niwe na wasiwasi. Mnaona?

Siasa; sasa tunachukua kama … Hebu na tuchukue kwa mfano … kuona kama watu wamekusudiwa kuwa katika tabaka tatu—tatu. Hebu na tuchukue siasa. Kuna wengine ambao wanampenda mtu huyo kupindukia. Na kundi lingine linamchukia. Na kundi lingine halijui la kufanya juu yake; hawajui ni upande upi, na linawaingiza kwenye machafuko.

*Mtu* huyu alisema, "Loo, yeye ni mtu mashuhuri. Yeye—yeye atatufaa kuwa Rais bora kuliko wote."

Yule mwingine akasema, “Yeye si kitu ila ni mhaini.”

Ndipo wale waliokuwa katikati wakasema, “Sasa sijui la kufanya.” Mnaona? Mnaona, tumeumbwa hivyo. Tumeumbwa hivyo. Hivyo ndivyo binadamu walivyo. Ilibidi iwe hivyo kutimiza uchumi mkuu wa Mungu. Na kufanya mafanikio Yake atakayofanikisha duniani, ilibidi mwanadamu aumbwe hivyo. Moja ni *kweli*. Yule mwingine *amekosea*. Na hilo lingine liko *katikati* ya hayo mawili. Daima imekuwa hivyo.

50 Angalia, wanafanya jambo hilo kila wakati ambapo hawajui… Angalia, wanafanya jambo hilo kila wakati ambapo hawajui…Mtu aliye katikati, ni mahali pabaya kwa sababu: mtu anaweza kuonyesha jambo hilo, kwamba ni kwa nini anafikiri yeye ni sahihi; huyo mwingine anaweza kuonyesha jinsi anavyofikiria amekosea; na yule aliye katikati hajui kitu juu ya jambo hilo, hajui ageukie upande gani. Na hivyo ndivyo ilivyo tu katika dini. Watu wanafanya jambo lile lile leo kuhusu mwisho wao wa Milele.

Sasa tutaumia, kwa dakika moja tu. Wanafanya hivyo kuhusu mwisho wao wa Milele. Mtu atashuka kuja hapa kwenye—kwenye hii … kula. Na kama ungepata buibui katika bakuli lako la supu, ungetaka kuishtaki kampuni hiyo au mkahawa huo. Mbona, usingekula supu hiyo, ingekuwa na sumu. U—u—u—usingeinywa hata kidogo, mende mkubwa ama kitu fulani kilichochemshwa katika bakuli la supu. Mbona, usingeinywa hata kidogo. Ingekuchefua kuwazia jambo hilo. Lakini hata hivyo, utaruhusu kundi la wanateolojia waingize kitu fulani ndani ya koo lako kitakachokupeleka maili milioni moja kutoka kwa Mungu, na unakimeza. Wakati, “Mtu ataishi kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Ni mnyororo ambao nafsi yako inaning'inia juu ya kuzimu nao. Na kama nilivyosema hapo awali, “Nyororo ni imara sana kwenye sehemu yake iliyo dhaifu sana.” Kiungo kimoja kuvunjika…hilo tu ndilo linalokupasa kufanya ni kuvunja kimoja; hivyo tu. Vingine vyote vinaachilia pamoja nacho. Ina nguvu tu kadiri ya kiungo chake kilicho dhaifu sana.

51 Sasa … Na mtu anayejua ya kwamba kama ukila supu hiyo iliyo na buibui mwenye sumu, labda itakufanya kuwa mgonjwa. Ingekubidi kwenda hospitalini, na—na tumbo lako lipigwe bomba na upitie katika usumbufu mwingi. Na ingeweza kweli kukuua. Lakini, jamani! Unge … Mbona, kamwe usingekaribia mahali kama hapo. Usingetaka kuukaribia huo mlango tena, kwa sababu u—u—unaogopa utatiwa sumu na kufa. Na halafu utajiunga kabisa, uandike majina yako kwenye vitabu, na kupingana hoja kile Biblia ilisema, “Haliuhukumu mwili wako, bali linaipeleka nafsi yako kuzimuni.” Mnaona? Ni ajabu jinsi gani watu wanavyofanya. Wao—wao wame … Wao huchukua kikomo chao cha Milele, wanakiweka msingi wake kwenye neno fulani la kitheolojia. Nawe unaweza kuwaletea Maandiko, kasema, “Hivi ndivyo Biblia ilivyosema. Hii hapa papa hapa.”

Naye mwanathiolojia ataliangalia, “Vema, hilo lilikuwa ni kwa ajili ya siku zilizopita.” Mnaona? Nawe unamsikiliza. Mnaona yale Mungu asemayo. Mkristo halisi, wa kweli husikiliza tu Neno hilo, na hivyo tu. Mtu wa Mungu huishi kwa Mkate huo.

52 Angalia, wengine—wengine wanaamini katika Neno. Wakati kuna wengine wanaoamini katika tafsiri yao ya kimadhehebu. Na kuna wengine, kwa mchafuko huu, ambao hawajui la kuamini.

Sasa *baadhi* yao walisema, “Loo, hili Baraza la Makanisa Ulimwenguni, hilo ndilo litakalokuwa jambo hilo. Litatufanya sisi sote kuwa kitu kimoja. Loo, hilo tu.”

Na wengine wanasema, “Mbona, ni wa ibilisi! Hili hapa katika Maandiko.”

Ndipo *mtu asiyechukua wakati* wa kuketi chini na kuomba na kutafuta, alisema, “Loo, sahau.” A-ha. Nisahau? Ni ninii yako…kwa tamshi lako, ndugu, kwa wadhifa wako, jinsi unavyolichukua, litakupeleka kwenye kikomo chako cha Milele ambako utakuwa daima. Usifanye hivyo.

53 Inatupasa kuketi wakati kitu kama hiki kitakapoinuka. Na swali, kama vile katika siku za Yesu; walipokuja, kanisa lilisema, “Loo, Yeye ni mwasi tu. Hakuna kitu Kwake.”

Lakini Mmoja alisema, “Yachunguzeni Maandiko.” Yeye alisema, “Ndani Yake unafikiri una Uzima wa Milele, nao wanakwambia Mimi ni Nani.”

Ndipo wanaume, wanawake, wakiwa na hadhi yoyote ya Kikristo hata kidogo, ama wanaopenda mwisho wao wa Milele, wanapaswa kuchunguza Maandiko na kuona kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Ndipo swali lisingekuwa, “Ni nani huyu?” Wangesema, “Huyu hapa!” Hiyo ndiyo tofauti. Mnaona, ni mwanadamu, wao—wao—wao wanaelekea tu kuwa hivyo. Wengine wamekusudiwa. Ni vigumu kusema hivyo, bali ni kweli. Inaonyesha jambo hilo. Mnaona?

54 Sasa, leo, wengine wanasema, “Ninaamini Neno. Neno ni Kweli; kila Neno Lake.”

*Wengine* wanasema, “Vema, wachungaji wetu wanaenda na kusomea ninii ya namna hiyo… Wanajua la kusema kuhusu Hilo.”

*Mwingine* akasema, “Vema, sijui. Nilijiunga na hili. Sikulipenda. Nilienda hapa na kujiunga na *hili*. Si—sijui nijiunge na lipi.” Mnaona? Hivyo ndivyo ilivyokuwa wakati huo, umati wa watu wa namna hiyo. Vema

daima imekuwa hivyo, tangu mwanzo, na daima itakuwa hivyo.

55 Sasa hebu na tuchunguze Kweli ya Biblia juu ya jambo hili, na tuone kama ni kweli; kwa dakika chache tu sasa … Adamu … Hapo mwanzo ilianza namna hii, jinsi tunavyolifanya siku hizi, haijabadilika hata kidogo. Adamu alikuwa "mwamini." Shetani alikuwa ni "asiyeamini"; hakuliamini Neno. Kwa hiyo akampata Hawa, ambaye "hakuwa na hakika" kama ilikuwa ni kweli ama si kweli. Mnaona? Shetani, asiyeamini … Mungu alisema, "Siku utakayokula, siku hiyo utakufa."

Shetani akasema, "Hiyo si kweli." Mnaona, naye hakuamini jambo Hilo. Adamu aliamini jambo Hilo. Kwa hiyo akafanyia kazi na yule aliyekuwa katikati. Wasingeweza tu kusema … yeye asingeweza tu kujua.

56 Sasa, angalia, mwanamke hapa anawakilisha kanisa la baadaye la kimadhehebu linaloitwa bibi-arusi. Yote yalikuja katika Mwanzo. Ni mbegu. Ukianzia katika Mwanzo; utapata picha yako sawasawa. Mnaona? Sasa, hapa, mwanamke aliwakilisha kanisa la siku hizi kwa sababu wengine wanasema (sasa hebu tuwachukue Wapresbiteri, na Walutheri, na wote hao wakija huku, hawa wafanyabiashara na kadhalika), "Tungependa kuwa na ninii… Tunataka ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tu—tungetaka kuupata."

Je! Mnatambua siku ambayo tungeweza kuwa ndani yake? Mnaona? Ingewezekana kuwa kwamba kamwe hawampati. Mnajua Yesu alisema, "Wakati wao, wale wanawali waliolala …"?

Sasa, kumbukeni, bikira aliyelala alikuja kuomba mafuta. Alifungiwa nje. Yeye hakuyapata. Yeye kamwe hakuyapata. Je! mnatambua ya kwamba Bibi-arusi akiisha kuondoka, kunyakuliwa kwenda Mbinguni, makanisa yangali yataendelea, watu wanafikiri wanaokoka na kila kitu kama tu walivyofanya sikuzote. Endelea tu kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu. Waliendelea moja kwa moja wakila, wakinywa, na kila kitu kama tu walivyofanya sikuzote. Hawakujua jambo hilo, bali mlango ulikuwa umefungwa. Na huenda ikawa, marafiki, ya kwamba mlango ungeweza kufungwa wakati wo wote. Labda tayari, kwa yote nijuayo. Hatujui.

57 Watakuwako wachache tu watakaoingia. Tunajua ya kwamba "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu (watu wanane waliokolewa), ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Kuna watu wachache tu watakaookolewa. Sisemi nane. Huenda ikawa mia nane ama … Si—sijui ni wangapi. Elfu nane … Si—sijui. Milioni nane … Mimi …

Lakini mnaona, Bibi-arusi hatafanyizwa tu kwa kundi dogo lililopo hapa duniani sasa. Wakati wa zamu ya saba, wakati Yeye alipokuja, hao mabikira wote waliamka na kutengeneza taa zao. Huko nyuma kabisa, kila mmoja aliyeamini Neno lililotiwa mafuta katika nyakati zote, alitokea. Kama vile piramidi (sehemu ya chini), na kuja juu … Lakini lile Jiwe la Kuweka Juu ilibidi lije kuchukua kitu hicho chote kulifanya pi—piramidi. Mnaona, kuliweka pamoja. Sasa, Bibi-arusi atafanywa na wale wote katika nyakati zote, ambao wamemwamini na wamemkubali Kristo kama Mwokozi wao.

58 Sasa, Hawa hakuwa na hakika. Adamu alimwambia, kasema, "Sasa, Mungu alisema, Mpenzi, kwamba, 'Siku utakayokula, siku hiyo utakufa.'"

Lakini wao walisema … Shetani alisema, "Hakika hilo haliwezi kuwa sawa. Unafikiria Baba—Baba angewatendea watoto Wake … Raha kidogo tu, kitu kama hicho. Hakika sivyo ilivyo." Mnaona?

Na hatimaye aligeukia nini? Aligeukia ile "hakika." Na hivyo ndivyo hasa kanisa linavyofanya leo, kabisa. "Loo, hakika … Sisi ni kanisa kuu. Sisi ni watu mashuhuri. Tumekuwako kwa muda mrefu … Upuuzi huu wote wanaouita ushupavu wa dini hapa nje, upuuzi hu—huu wanaouita ubatizo wa Roho Mtakatifu na kadhalika, huo ni upuuzi! Mnaona, hiyo … Hakuna kitu kama hicho. Ah, hakika … Ninatoa zaka. Ninaenda kanisani. Mama yangu alienda kwenye … Hakika Mungu …" Lakini, Mungu alisema tofauti, na hivyo ndivyo itakavyokuwa, kwa ladha tu ya Neno Lake. Yeye alisema jinsi wakati huu wa kanisa la Laodikia ungekuwa. Nina kitabu maalum kinachotolewa, juu yake, hivi karibuni sana, Bwana akipenda, unaona, juu ya Laodikia hii, kuonyesha ya kwamba tayari imekwisha, ya kwamba tayari ametiwa muhuri mle ndani, na Kristo yuko nje. Kamwe halikusema alirudi akaingia ndani tena, wajua. Kwa hiyo tunaona jambo hilo leo, wakilitoa Neno nje, kama tu ilivyokuwa sikuzote.

59 Sasa, angalia, Musa, Neno lililotiwa mafuta … ama ama tunamwita … Natumaini mtaelewa, nitakaposema ya kwamba yeye alikuwa ni Masihi. Yeye alikuwa Neno lililotiwa mafuta lililokuwa limeahidiwa kwa ajili ya siku hiyo. Musa alikuwa hivyo! Mnaamini jambo hilo? Hakika, neno—neno Masihi linamaanisha "aliyetiwa mafuta." Mnaona? Sasa, Nuhu alikuwa ni *mtiwa mafuta* wa siku yake. Ibrahimu alikuwa amesema ya kwamba kungekuwa … Watu wake wangekaa ugenini miaka mia nne, nao wangetolewa kwa mkono wenye nguvu, na yale angeonyesha: ishara zake na maajabu … na—na vizazi vilivyokuwa vikija, na yale yangetendeka. Naye Musa akasimama pale, hilo *Neno lililotiwa mafuta* la siku hiyo. Hiyo ndiyo sababu angeweza kuweka mkono wake kifuani. Kwa nini? Alikuwa amesimama katika Uwepo wa Mungu. Amina! Utukufu mkuu wa Shekina ukimzunguka. Kila hatua aliyofanya ilimwakilisha Mungu. Hapo ndipo kanisa linapopaswa kusimama sasa. Sawa! Badala ya jambo hilo, tumeingia kwenye ghadhabu ya kitu fulani cha kimadhehebu.

60 Lakini Musa alikuwa amevutiwa, naye akaja kando. Na kulikuwa na ile Nguzo ya Moto ikining'inia pale kwenye kile kijiti. Na hapa alisimama Musa aliyetiwa mafuta. Hapana shaka mtu huyo hata hakujua alichokuwa akifanya. Ishara alizopewa aliposimama pale pamoja na fimbo yake ya mchungaji, na kujua ya kwamba hiyo ingekuwa ni fimbo jangwani. Iligeuka ikawa nyoka, kisha ikawa upatanisho; ndivyo alivyofanya huyo nyoka, huko jangwani. Mambo yote aliyofanya … Yalikuwa ni ishara na sauti zikinena na hao watu. Mnaona, kulikuwa na kitu kilichounganishwa naye. Na huenda Musa hata hakujua jambo hilo mwenyewe, bali yeye alikuwa ni Neno lililotiwa mafuta la siku hiyo. Yeye alikuwa ni Mjumbe aliyetiwa mafuta. Kwa hiyo kama alikuwa ndiye Mjumbe wa wakati huo, yeye alikuwa ndiye Masihi wa wakati huo. Yeye alikuwa ndiye aliyetiwa mafuta.

Sasa, yeye, Yoshua, na Kalebu, walikuwa waaminio katika kundi hilo (angalia) na walijaribu kuwafundisha wengine Kweli. Lakini mnaona, Shetani (Dathani na Kora) waliwafanya wengine kuangamia jangwani. Sasa, shida ilikuwa ni nini?

61 Mungu alikuwa amemwita Musa. Hakutaka kwenda. Hao manabii walikuwa na mambo kama hayo ya kufanya mpaka wao—wao … Lilikuwa ni jambo gumu kufanya. Hawakutaka kutoka nje, na kudharauliwa. Walitaka kuwa na ushirika na kuingia pamoja na hao wengine na—na kwenda pamoja na ndugu. Lakini unaona, kama tu vile…ninaamini…ninasahau ilikuwa ni nabii yupi, aliyesema, "Kama…sitaki kufanya jambo hili," (kwa maneno mengine) "lakini moyo wangu wote utashika moto. Mungu amenena nami sina budi kulipeleka." Kama walilipenda; kama watu walimsulibisha; kama walimpiga kwa mawe; lolote walilofanya… Mungu amenena moyoni mwake, naye hana budi kulisema. Si kuwa tofauti, bali kuwa mtiifu. "Kutii ni bora kuliko dhabihu; kutii, kuliko mafuta ya kondoo dume." Mnaona, lilikuwa moyoni mwake. Hana budi kufanya hivyo. Yalikuwa ndiyo Maisha yake. Asingeweza kulizuia. Kulikuwako na kitu fulani, mdundo fulani, ulioyasukuma. Wasingeweza kulibariki wala kulilaani. Mungu alikuwa na mamlaka kamili juu yao mpaka Yeye—Yeye alikuwa ni sauti yao, tendo lao. Haleluya!

Nipe Kanisa lililotiwa mafuta chakari na Mungu mpaka kila tendo lao na hatua yao ni BWANA ASEMA HIVI, linalotembea katika huo Utukufu wa Shekina, nitawaonyesha Masihi (mtu wa Mungu aliyetiwa mafuta) anayesimama juu ya nchi.

62 Hapo alisimama Musa karibu na kijiti hiki kilichowaka moto na Utukufu wa Shekina. Alisimama pale, ametiwa mafuta, ilikuwa ni vigumu kwake kujua alilokuwa akifanya. Alikuwa tu akitii kile ile Sauti ilichosema afanye, "Weka mkono wako kifuani mwako. Utoe. Chukua hiyo fimbo. Igeuze iwe nyoka. Itupe chini tena." Haidhuru mtu mwingine yeyote alisema nini, yeye alikuwa akifanya jambo hilo.

Kasema, "Bwana, nionyeshe Utukufu Wako, nami niko tayari kwenda Misri. Siwezi kuzungumza vizuri. Siwezi kuzungumza vizuri. Lakini Wewe uniruhusu nione Utukufu Wako." Naye akamwonyesha jambo Hilo. Naye akashuka akaenda na kuchukua mambo haya haya, na kuonyesha ya kwamba yeye alikuwa ndiye Masihi aliyetiwa mafuta. Mtu huyo aliokota mavumbi kutoka ardhini na kuyatupa hewani, na nzi na viroboto wakaruka kutoka kwenye mavumbi hayo, na kuifunika nchi. Ni kitu gani kingeweza kuumba, ila Mungu? Alichukua maji kutoka mtoni na kuyamwaga ukingoni; na kila tone la maji kote Misri, likageuka kuwa damu. Ni kitu gani kingeweza kufanya jambo hilo, ila Mungu? Ilikuwa ni kitu gani? Yeye alikuwa amejitolea kabisa kwa Neno la Mungu lililotiwa mafuta hata alikuwa Masihi.

Wamisri walijaribu kulikataa namna hii … Wasioamini walijaribu kulikataa. Waamini wa kujifanya walijaribu njama zao. Lakini Neno la Mungu liliwapeleka moja kwa moja hadi kwenye Nchi ya Ahadi. Hiyo ni kweli. Walikuwa wametiwa mafuta. Walikuwa … Yeye alikuwa Masihi.

63 Sasa swali linakuja huko nyikani. Hapa ndipo linaposababisha… Mnaona, sasa, ninawatakeni mwangalie, ndugu zangu. Sasa kumbukeni, watu hawa walifurahia baraka hizo. Walifurahia mahubiri ya nabii huyu, huyu mtiwa mafuta. Walimwamini. Walimfuata. Lakini kulitokea nyikani, mmoja jina la—lake Dathani, na mmoja jina lake Kora. Nao wakasema, "Hili halina budi kuwa ni jambo la mtu mmoja. Musa anadhani yeye ndiye tu aliyeitwa na Mungu."

Ujumbe huo wa mtu mmoja, hawakuutaka. La, hawakuutaka. Na Mungu kamwe hakushughulika ila na mtu mmoja kwa wakati mmoja. Daima ni Ujumbe wa mtu mmoja. Ni lini Yeye aliposhughulika na watu, nje ya mtu mmoja tu? Ni mtu binafsi. Si kundi. Mnawajibika kwa Mungu, kila mmoja wenu. Unasema, "Loo, ninaamini." Unaninii tu … Kile unachofanya, unalifurahia tu. Unafurahia wazo fulani.

64 Huyu hapa mwanamke amesimama hapa. Mimi ni kijana mwanamke, nikingojea kuolewa. Analingana matakwa yangu kwa kila njia. Yeye ni Mkristo mzuri; anaonekana hivyo, anavaa hivyo, anaenenda hivyo, anaishi hivyo. Nitakubali atakuwa mke mzuri kwangu. Bali yeye si wangu mpaka nitakapomchukua awe wangu.

Hivyo ndivyo Ujumbe ulivyo. Unaweza kuhurumia na kusema, "Ni kweli." Bali inakubidi kuuchukua wewe mwenyewe upate kuwa sehemu Yake. Ndipo wewe na Ujumbe mnakuwa mmoja. Kisha upako uko pamoja nawe, kama ilivyo kwa hao wengine.

65 Sasa, Shetani, hakuamini jambo Hilo. Dathani … Alimfanya Dathani na hao wengine wasiliamini, akawafanya wote waangamie.

Lakini unasema, "Ngoja kidogo, Ndugu Branham, ulisema, 'Watatu: Musa, Yoshua, na Kalebu.'" Hiyo ni kweli kabisa. Hivyo ndivyo ilivyokuwa. "Lakini hapa unasema tu, 'Wawili.' Mnasema hapa kwamba 'Kulikuwa na …'"

Unasema, "Shetani wa kimiujiza." Lakini kulikuwako na Mungu wa kimiujiza, pia, akiwatia mafuta hawa watatu. Sasa, Shetani ametiwa mafuta tu. Lakini huyo mwingine anakuja, huyo mwingine anakuja, angalieni tu kwa dakika chache. Yeye anajitokeza jukwaani, jina lake ni Balaamu. Yeye ni nabii anayependa fedha; anayejiita nabii, nabii wa uongo.

66 Daima kuna kila namna ya manabii. Na daima pamoja na Israeli na pamoja na hilo kundi, daima kulikuwako na manabii; hao: manabii mororo, manabii wa kujipendekeza, ambao walitembea na kutaka kujipendekeza kwa mfalme, na kupata riziki, na, vema, kama vile Ahabu alivyokuwa na hao mia nne, wote wamevalia mtindo wao wa kikasisi. Naye akawaambia … alimwambia yule—yule—yule mfalme mkuu kule juu, Yehoshafati, akasema, "Mbona, hakika, nina watu mia nne, wote waliofunzwa vizuri, manabii wa Kiebrania."

Nao wote walikuja na kutabiri. Lakini mtu huyo alikuwa na Mungu wa kutosha ndani yake kujua ya kwamba hilo lilikuwa ni kosa, maana alijua Eliya alikuwa amelaani kitu hicho. Na Mungu angewezaje kubariki kile alichokuwa amelaani? Asingeweza kufanya hivyo. Akasema, "Je! Una mmoja zaidi tupate kuuliza?"

Yeye alisema, "Naam, una mmoja hapa nje; Mikaya, mwana wa Imla. Lakini," kasema,"ninamchukia." Kasema, "Yeye anatuingilia sikuzote akinilaumu na kuninenea kila kitu kiovu." Ingewezekanaje … Simba alikuwa amenguruma. Mungu alikuwa amenena. Ni nani asingeweza kusema Kweli? Wakati ilikuwa ni kinyume cha Neno la Mungu, ilibidi akilaani kitu hicho. Daima wamekuwa na huyu, nabii wa uongo. Lakini wamekuwa na wa kweli daima, pia. Kumbukeni, hapakuwa na shule nzima yao. Kulikuwako na mmoja wao. Na hivyo ndivyo ilivyo katika siku yoyote. Hivyo ndivyo ilivyo, leo.

67 Nabii wa siku hizi ni Neno hili. Hiyo ni kweli. Nabii, leo, si wote hawa hapa tofauti … Kuna nabii wa Kimethodisti, nabii wa Kibatisti, nabii wa Kipentekoste, kila namna ya manabii kila mahali, kote nchini. Lakini bado inabakia: kuna nabii Mmoja wa Kweli, yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Yesu Kristo! Naye ni Neno. Hiyo ni kweli. Yeye ni Neno: Neno lililotiwa mafuta la wakati huu.

68 Mwangalie sasa, tunaposafiri. Tunaona ya kwamba Yoshua na Kalebu … Na kisha huyu hapa Balaamu anakuja katika nabii wa kukodiwa. Alifanya nini? Alikanyaga moja kwa moja juu ya kila Neno la Mungu, baada ya Mungu kumwonyesha. Yeye anawakilisha madhehebu, leo. Tutaonyesha jambo hilo katika dakika chache tu; Dathani, kile alichokuwa, na vile hao wengine walivyokuwa. Sasa Balaamu aliwakilisha madhehebu. Mtu asiyepaswa … anapaswa kujua vizuri zaidi. Alijua hilo lilikuwa ni kosa. Lakini alifanya nini baada ya jambo hilo? Mungu alimpa onyo, na bado alikanyaga moja kwa moja kwenye hilo onyo. Alikuwa ana wazimu mwingi mno wa fedha na kupendwa na watu sana kwamba aliweza kuwa ni wa kundi lao. Na ndivyo makanisa yanavyofanya leo, wakiingia moja kwa moja kwenye hilo Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Na kila onyo linaenea kote nchini, na ishara na maajabu katika siku hizi za mwisho. Wanatembea na kuingia moja kwa moja ndani yake hata hivyo, kwa sababu wanapenda kusifiwa na wanadamu zaidi kuliko wanavyolipenda Neno la Mungu.

69 Nina rafiki mzuri huko nje, anayehubiri ujumbe huo; Mpentekoste, akiwa huko nje akiwaambia watu, akijaribu kuliunganisha kanisa pamoja. Akisema ya kwamba, "hatuna budi kuingia ndani ya huu, uamsho huu wa ekumeni." Mbona, baadhi yao … kanisa la Kristo. Mengi ya madhehebu haya ambayo hata hayaamini katika kuzaliwa na bikira, na mambo hayo yote mbalimbali, na wote ni wanachama wa huo. Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipopatana? Halafu, ulisema, "Amina" kwa jambo hilo, sijui juu ya jambo hili sasa: Basi mtu anawezaje kusema ya kwamba yeye ni Mkristo na amejazwa na Roho Mtakatifu, na akane ya kwamba Neno hilo ni lile lile jana, leo, na hata milele? Roho Mtakatifu ndani yako ataliweka hilo Neno, kila Neno, "Amina. Amina. Amina." Wakati Neno linaposema jambo lo lote, unasema, "Hiyo ni Kweli." Amina! Ninii … maana mnakubaliana na Neno. Umepatana na Mungu. Wewe na Mungu ni mmoja. Mungu yuko ndani yako. Wewe ni mwanawe ama binti Yake, anakufanya masihi Wake, Neno lililotiwa mafuta likiishi ndani yako.

70 Angalia, Balaamu alitembea moja kwa moja kuvuka mambo haya. Yeye alikuwa dhehebu kamilifu na jibu kamili kwa ladha yao. Hivyo ndivyo Dathani alivyotaka. Hivyo ndivyo Kora alivyotaka. Walitaka kuunda madhehebu kutoka kwake. Kasema, "Tuna watu watakatifu kote hapa."

Sijali jinsi watu wawili wangetembea pamoja kikamilifu, kuna tofauti yao. Pua zetu hazifanani. Picha zetu za vidole gumba hazifanani. Kuna mambo mengi kutuhusu … Hata hivyo tunaweza kupeana damu mmoja kwa mwingine, hata katika mapacha, na bado ni tofauti. Basi, mnaona, Mungu anamweka mtu mmoja tu katika mdundo huo, na wengine wanamwamini huyo.

71 Yeye alimfanya mtu mmoja, na watu wengi kutoka kwa mtu huyo. Kama vile wote wanavyokufa katika Adamu, wote wanaishi katika Kristo. Yeye alifanya njia moja ya mauti, nao wote wakaingia humo. Naye alifanya njia ya Uzima, na wote wanaoiendea wana Uzima. Kutoka kwa Mtu mmoja, si watu dazeni moja walikuja na wakafa. Watu kumi na wawili hawakulazimika kutenda dhambi. Mtu mmoja alitenda dhambi moja. Mtu mmoja alilipia adhabu kamili. Mtu mmoja alilipia adhabu yote. Haihitaji kutambaa tena kwa magoti yako, na kusema Salamu Maria, na aina yote hii ya mambo, na kulipa sadaka za wafu. Yesu alikufa ili Kipawa cha Mungu kiwe huru. Alilipa deni kamili. Lakini mnaona, tunataka kuwa na jambo lingine la kusema ndani Yake.

72 Angalia jambo hili sasa. Hawa jamaa walikwenda pale na kusema, "Vema, unajaribu kujifanya mtu wa pekee katika kundi hilo. Unafikiri wewe ndiwe pekee."

Ndipo Moses alichoshwa naye. Alirudi, akasema, "Baba …"

Yeye alisema, "Jitenge nao. Ni—ni—ni …"

"Wote—wote walio upande wa Mungu, njooni huku." Naye akaifungua nchi na kuwameza. Hiyo ni kweli? Hebu wazia tu jambo hilo, ndugu. Loo, jamani! Kwa nini hawakumwamini? Kwa nini hawakuamini ya kwamba—ya—ya—ya kwamba Musa huyu alikuwa ni yule kiongozi, wa Mungu? Kwa nini walitaka kuzozana naye? Daima wananung'unika na kulalamika, walipoona mkono wa Mungu na kusonga chini ya … Naye Musa … Mungu alikuwa amethibitisha ya kwamba—ya kwamba Musa alikuwa ni Masihi Wake aliyetiwa mafuta. Mnaona? Halafu basi … Mnaona, ndani ya moyo wao, walikuwa wakitaka kitu fulani tofauti.

73 Ni kitu gani kilichowapata ninyi Wapentekoste? Miaka michache iliyopita mlitoka kwenye machafuko hayo yanayoitwa madhehebu, kujifanya Wapentekoste. Kwa nini mlitaka kurudi ndani yake tena? Ganda lilipaswa kuja. (Punje haikuwa hapa, bado.) Mnaona? Angalia, hivyo ndivyo walivyofanya tu. Hilo lilikuwa moyoni mwao. Iliwabidi kufanya hivyo.

Sasa, mnaona, Dathani alikuwa na wazo la kwamba wote wangeweza kuunda dini kubwa kutoka kwake. Mwajua, hata mtume Petro alikuwa na wazo lile lile kwenye Mlima wa Kugeuzwa. Yeye alisema, "Na tujenge vibanda vitatu hapa; kimoja cha Musa, na kingine cha torati, na kimoja kwa ajili ya manabii, kimoja…"

Na wakati alipokuwa bado anaongea, ilisikika Sauti, ikasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa. Msikieni Yeye." Hapo ndipo walipotazama nyuma, walimwona Yesu pekee. Hapo Yeye alisimama. Yeye alikuwa Neno. Hilo tu ndilo unalopaswa kusikia, ni hilo Neno. Huyo ni Yeye katika wakati wowote. Angalia kile Neno linachosema kwa ajili ya wakati huo, na mwangalie Mungu akilitia mafuta, na uambatane Nalo. Hivyo tu.

74 Waliifuata ile Nguzo ya Moto hadi kwenye Nchi ya Ahadi. Wale waliomaliza safari waliifuata, hao wengine wakaangamia. Angalia, walitaka Neno lichanganyike na ulimwengu … liliwafanya wakosee. Na angalia vile lilivyowafanyia. Neno … Walilikosa kwa maana wasingekubali Neno lililotiwa mafuta. Mnaona, huna budi kuwa na bandia … Kwanza huna budi kuwa na kitu halisi, kufanya bandia yake. Na hapo walikuwa nayo, na Mungu alionyesha ya kwamba Yeye hakuwa pamoja nayo.

75 Wazia jinsi Neno lilivyokuwa limefanywa kamilifu kwao, kwa kuthibitishwa kwao. Kila kitu ambacho Musa alitabiri kingetukia. Kwamba alikuwa amewaita kuwapeleka kwenye Nchi hii ya Ahadi. Kila kitu ambacho Musa alitabiri kilitukia, papo hapo. Hakuna Neno Lake lililoshindwa. Ni majaliwa jinsi gani kwamba hayo yalipaswa kuwa, kujua ya kwamba mlikuwa mkitembea jangwani… Na hapo, baada ya … Wakati alipowaambia Ujumbe, iliwabidi kuuamini kwanza. Lakini baada ya kuwatoa kule, ndipo Mungu akasema, "Nitawathibitishia ya kwamba Mimi ndiye ile Nguzo ya Moto mliokutana nayo jangwani."

Kwa hiyo akasema, "Wakusanyeni wote pamoja mlimani." Naye akashuka juu ya Mlima Sinai. Ndipo Mungu akaanza kuunguruma.

Nao watu wakasema, "Usimwache Mungu azungumze. Acha Musa azungumze. Usiruhusu …"

Mungu alisema, "Sitasema nao tena namna hii, bali nitawainulia nabii atakayenena katika Jina Langu." Mnaona? Kwa hiyo tunaona ya kwamba hivyo ndivyo Mungu amefanya daima. Kwa nini hawakuweza kuona jambo hilo hapo mwanzo? Kuona mambo haya yote, na kisha wanung'unike dhidi ya Ujumbe uliokuwa ukiwapeleka kwenye Nchi ya Ahadi; walioanza nao ipasavyo, na ukiwapeleka kwenye Nchi ya Ahadi. Lakini wao bado … iliwabidi kunung'unika dhidi Yake. Wazia, jinsi walivyokuwa wakamilifu … jinsi ambavyo wangeweza kutembea kila siku, wakitembea pamoja na Bwana. Ni maisha ya jinsi gani kuishi, moja kwa moja jangwani! Wakati wa usiku … Kuleni mana asubuhi, iliyoanguka usiku.

76 Mnajua, lilikuwa ni la kawaida sana kwao hata wakasema, "Nafsi yetu inakinai Chakula hiki." Mnaona? Na hivyo ndivyo imekuwa kwetu. Ninafikiria tu juu ya makundi madogo ambayo sisi … katika huduma yangu ndogo, kote nchini. Kuona si uponyaji tu na kadhalika; hilo limekuwa hivyo daima. Kuponya; Mungu

daima alikuwa na njia ya kuponya mahali fulani. Hata Yeye alikuwa na M—M—Malaika kwenye kidimbwi wakati mmoja. Naye … kila namna ya mambo. N—nyoka wa shaba jangwani. Daima umekuwa na ishara za uponyaji. (Hicho sicho ninachozungumzia habari zake.) Uponyaji ni jambo moja linalovutia usikivu wa watu. Mtu yeyote atatoa sadaka kwa ajili ya ibada ya uponyaji. Wata—watatoa kwa ajili ya sikukuu ya nyimbo. Lakini inapofikia maskini nafsi iliyopotea, hawana uhusiano wowote na jambo hilo. Mnaona, sasa hiyo si ni sawa? Tuna kila kitu … kwa maskini nafsi iliyopotea. Usitake uhusiano wowote na jambo hilo. Watamwacha apapase katika kitu chochote. Sema, "Vema, hilo ni sawa, yeye ni mfuasi wa kanisa. Haitadhuru chochote."

77 Lakini sasa, tunaona hapa … (Tunakaribia kufunga upesi tuwezavyo hapa.) Wazia jinsi ilivyokuwa kamilifu. Ninaangalia kote katika zile—zile siku ambazo tumekuwa hapa duniani. Angalia yale Bwana Mungu amefanya. Alianza na ishara kubwa, na maajabu, na miujiza, ambayo sote tulifurahia. Kisha angalia … Ndipo unakuja Ujumbe nyuma yake.

Angalia kilichotukia. Ukitembea, si peke yako tu, mtu fulani akiambatana nawe. Mnaona kundi la Malaika wakitoka Mbinguni, wakiitikisa dunia nzima, unasimama tu pale. Na magazeti yanaandika habari zake; wakati imetabiriwa miezi na miezi hapo nyuma jambo hilo lingetukia. Hapo Yeye alisimama pale, na kusema, "Wakati umewadia, rudini. Fungua ile Mihuri Saba ya siri ambayo ilikuwa imefichwa kote kupitia yale matengenezo na kadhalika, uielezee." Halafu kunakuja kuhubiriwa kwa *Uzao wa Nyoka*, na mambo haya yote namna hiyo. Na makasisi hufanya nini? Badala ya kusema … "Mbona, Luther alisema *hili* ama *lile*." Wao wananinii tu … Kamwe hawataliona. Mnaona? Lakini ni majaliwa jinsi gani kwetu sisi tunaoamini; kutembea katika Uwepo wa Mungu, kila siku.

78 Simama pale na uone upepo wa kisulisuli ukitoka angani. Ulikata mlima nusu vipande viwili, tukisimama pale mahali tulipokuwa; ukakata vilele vya miti na vitu kama hivyo. Ndipo mlipuko wa Neno ukatokea na kupatikisa mahali pale mara tatu, kasema, "Angalia ukielekea kwenye Pwani ya Magharibi." Ukaenda moja kwa moja kule na kutikisa Alaska. Na unakaja moja kwa moja kwenye Pwani ya Magharibi sasa. Ni kweli kabisa.

Siku iliyotangulia, nilichukua jiwe na kulitupa hewani, na kusema, "BWANA ASEMA HIVI, 'Wakati umewadia, hukumu zitaanza duniani. Matetemeko ya nchi na kila kitu vitakuwa vikitukia. Na Pwani yote ya Magharibi itatikiswa na kadhalika.'" Angalia jinsi lilivyo kamilifu. Siku baada ya siku, kila kitu jinsi hasa alivyosema. Tunawezaje kulikataa hilo, ndugu? Hebu na tushikilie imani yetu Kwake.

Wanasema, "Ni nani huyu?" Tunajua Yeye ni nani. Ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, ile Nguzo ya Moto. Wakati wa Musa, angalia kile alichofanya; mfano wa ile Nguzo ya Moto leo. Daima ni … Kwa nini hawakumwamini Yesu kuwa ni Neno? Walikuwa na tafsiri mbaya na ufahamu. Kama tu vile Hawa alivyofanya, ndivyo wanavyofanya sasa.

79 Ndipo Balaamu na fundisho lake lilikuwa sawa kwao. Nao walikidhi ladha yao hasa. Kwenye ile karamu, angalia … Kwenye Sikukuu ya Wamoabu, ona … Loo, yale aliyosema. Angalia hapa jinsi hilo lilivyokuwa na picha ya siku hizi, jinsi linavyoonyesha mfano wake huko nyuma. (Ninawaweka muda mrefu sana.) Lakini angalia, angalia, kwa muda kidogo tu, Sikukuu ya Wamoabu. Mnaona, kama Yeye asingewatoa moja kwa moja kutoka pale kwa njia moja, Balaamu aliwatoa, ndipo akawaunganisha pamoja. Kama hangeweza kuwalaani yeye mwenyewe … Kadiri alivyozidi kulaani, ndivyo Mungu alivyobarikiwa. Aliweka tu …

80 Mnaona, hivyo ndivyo alivyowafanyia Wapentekoste. Walisema miaka michache iliyopita, wakati ninyi nyote mlipoanza, "Msingefika popote. Hakukuwako na cho chote kwenu. Ninyi, mngeisha kabisa. Ninyi ni kundi tu la ushupavu wa dini." Lakini kila wakati walipokazana kuwalaani, mlirudi moja kwa moja tena. Mungu aliendelea kufunua Ujumbe Wake. Kutoka huko chini kwenye Assembly ya kale, huko nyuma kabisa mwanzoni, lile Baraza Kuu. Ndipo Yeye akauingiza wakati walipolipokea Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ubatizo wa maji. Ndipo mmoja akarukia upande huu, na huyo mwingine upande ule, na mmoja akaondoka…; akaunda *hili* na *lile*. Mungu aliendelea kubariki.

Sasa, vema, aliona asingeweza kuwalaani ninyi. Mnaona? Kwa hiyo atafanya nini? Yeye atawaundia dhehebu. Awalete … "Loo, sisi sote ni mmoja hata hivyo." Mnaona? "Sote tunamwamini Mungu yule yule." Kwa hiyo hivyo ndivyo alivyofanya Balaamu. Na je, Yuda hakutuonya juu ya jambo hili? Walikosea katika njia ya … katika mafundisho ya Balaamu na wakaangamia katika maasi ya Kora. Je, Yuda, ndugu wa kambo wa Yesu, hakutuonya juu ya jambo hili katika Biblia? Wao ni kama Kaini, tangu mwanzo, watu wa kukodiwa. Yule aliyeenda kanisani na kujenga makanisa na—na kujenga madhabahu na kutoa dhabihu. Wanakosea katika njia ya Kaini. Walikimbia katika njia ya Balaamu, wakaangamia katika maasi ya Kora. Yuda anaweka jambo lote dhahiri kama tu tunavyofanya asubuhi ya leo, hapa mbele yenu, kama vile ambavyo tumekuwa tukilifanya. Jambo lote liko pale.

81 Waliangamia katika maasi ya Kora. Wazia tu jambo hilo, jinsi hilo lilivyokuwa baya. Kufikiria tu juu ya kile Kora huyo … Mnaona, yeye alisema, "Sasa, sote tutaenda kwenye karamu. Sisi sote ni mmoja." Wamoabu walimwamini Mungu. Hao walikuwa watoto wa binti ya Lutu. Mnaona? "Sote tunaamini katika Mungu mmoja." Kimsingi, walikuwa sahihi kabisa. Mwangalie Balaamu kule juu, akiwa wa kimsingi kabisa

kama Mbaptisti yeyote mzuri ama Mpresbiteri siku hizi. Yeye alikuja pale na kulikuwa na Israeli, ambao hawakuchaguliwa … Wao walikuwa taifa. Israeli haikuwa taifa. Ilikuwa ni watu wakati huo. Hawakutaka kufuata njia ya Mungu, baada ya kitambo kidogo. Walitaka kuwa kama mataifa mengine. Hapo ndipo wanaposhindwa. Lakini mradi tu wanataka kukaa na Mungu, vema.

82 Balaamu akatoka, akaangalia chini, akasema, "Vema, jamani! Ninajua mmoja wa hao wahudumu alioa mke wa mtu mwingine." Mambo haya mengine yote, loo hakika, walikuwa na mengi sana. Alisahau kusikia kupaaza sauti kwa—kwa Mfalme kambini. Yeye kamwe hakuona ule Mwamba uliopigwa, na yule nyoka wa shaba akining'inia pale kwa ajili ya upatanisho. Hakutambua ya kwamba hawakuwa wamejiunga na dhehebu lolote. Walikuwa wameunganishwa kwenye Agano la Mungu, nao walikuwa wakitembea katika hilo. Mnaona? Naye Balaamu akasema, kimsingi, "Nijengee madhabahu saba." Hilo ndilo Yehova alilotaka. Hilo ndilo Yehova alilopata pande zote mbili. "Vema, weka ndama saba juu yake." Hivyo ndivyo walivyokuwa wakifanya kule kwenye kambi hiyo. "Niweke kondoo dume saba juu yake kwa sababu Masihi yuaja siku moja." Vema.

83 Mnaona, kimsingi, wote wawili walikuwa sahihi; kimsingi. Mnaona? Lakini siku moja alipoona asingeweza kumfikisha kwenye jambo hilo, alisema, "Kama tungejipanga tu pamoja basi." Na hapo ndipo walipofanya kosa lao.

Na hapo ndipo hasa Pentekoste ilipofanya kosa lake; wakati ulipounda madhehebu kama makanisa mengine. Mimi si adui yako. Mimi ni ndugu yenu. Baadhi ya siku hizi mtatambua ya kwamba hiyo ni kweli. Huenda ikachukua muda kidogo bado, kutua mara chache kwa jua, lakini siku moja mtaona ya kwamba hiyo ni kweli.

Ndipo fundisho la Balaamu likawapiga tu… Hivyo ndivyo walivyotaka. "Sisi sote ni mmoja." Mnaona? Kwa hiyo, hao hapo wakaenda. Manabii wao wote na wote walienda moja kwa moja pamoja nao. Naye alikuwa kwenye karamu, yeye yule alisema, "Nasi sote tunaamini ya kwamba kuna Mungu mmoja. Hebu na tuamini." Ni kile tu wangekuwa wakitafuta, hasa kabisa.

84 Sasa wakati Methodisti na Baptisti inapokuwa ni vigumu kwao kukusanyika pamoja kwa ajili ya madhehebu yao, lakini wakati shirika kubwa mno litakapokuja, ambapo sote tunaweza kuungana pamoja, vema. "Loo," unasema, "Wapentekoste hawatalipokea kamwe." Hawawezi? Wangefanya nini hivi majuzi huko Missouri? Mlisoma magazeti yenu, hakika. Mnaona? Hamtalipokea? La, si ninyi Wapentekoste, ninyi watu; lakini sio ninyi, ni ule utawala pale juu unaowasukuma. Hicho ndicho kichwa kinachowageuza. Hiyo ni kweli. Msiambatane nacho. Wewe kaa mbali na kitu hicho, hiyo ndiyo alama ya mnyama. Tokeni kwake upesi mwezavyo. Mnaona? Huo ni ukasi- … Hicho kichwa cha utawala ndicho kinachoendesha.

85 Wala tusingalitoka kwenda huko na kufanya vita na Ujerumani wala yo yote ya haya mengine. Tulikuwa na hawa…baadhi ya wanasiasa hawa wakubwa wanaoketi hapa kutengeneza bunduki mpya na kuanza… Sitaki fedha kutokana na…fedha za damu kutoka kwa mtoto wangu mwenyewe, ambaye inambidi kutoka kwenda huko na kufa kwa ajili yake. Mnaona? Lakini hivyo ndivyo ilivyo, siasa ndizo zinazofanya jambo hilo. Na ulimwengu mzima unatawaliwa na Ibilisi. Hivyo ndivyo Yesu alivyosema hasa. Na haitakuwa sawa mpaka ule Utawala wa Miaka Elfu, wakati Yesu atakapokuja na kutawala. Lakini sasa tunapata shida hizi. (Tuharakishe ili tupate kumaliza sasa.)

86 Kile tu walichokuwa wakitafuta…kitu chenyewe hasa. Hivyo ndivyo walivyotaka. Ushindi wa Shetani kwenye Karamu ya Wamoabu. Ana mwingine unaokuja, pia. Yeye anawaweka wote kwa njia ile ile. Ngoja … Mara moja! Wazia tu yale waliyofanya. Kama vile ilivyokuwa. Haikubidi kuchukua miaka mitatu ama minne mikubwa, mirefu, kulipanga. Wao…huyo nabii wa uongo, mtu aliyetembea juu ya Neno la Mungu… kila onyo ambalo Mungu ametuma kote nchini, na kuwaambia, "Tokeni kwake! Tokeni kwake! Tokeni kwake!" Hawatatoka. Watakaa papo hapo.

Wanalipuuza Neno la Mungu, wanapuuza Maneno, wanapuuza ishara, wanapuuza mambo yale tuliyo nayo. Na kuendelea moja kwa moja, "Tutalipata hata hivyo. Tunaendelea moja kwa moja. Hatuna budi kuwa nalo. Hivyo tu. Sisi sote ni mmoja." Mnaona upumbavu wa ibilisi? Walifanya jambo lilo hilo kwenye ile Karamu ya Nikea, huko Nikea, Urumi. Waliunda madhehebu kutoka kwake, na hilo ndilo lililotukia. Shetani alikuwa na Sikukuu ya Nikea. Loo, jamani! Na tangu wakati huo … Sikilizeni, nitasema neno kubwa mno hapa sasa. Na ninyi mlio kwenye kanda ambao mnataka kubishana juu ya jambo hili, mjadili wenyewe, na historia, na Biblia, mnaona, bali si kwangu mimi.

87 Sikilizeni! Kila wakati Mungu anapomtuma mjumbe na kuanzisha Ujumbe … Na wakati kanisa hilo, wakati kundi hilo la watu linapoingia kwenye karamu ya kimadhehebu … Hapo ndipo wanapofanya jambo hilo. Hapo ndipo ninyi Assemblies mlipofanya jambo hilo. Hapo ndipo ninyi Oneness mlipofanya jambo hilo. Hapo ndipo ninyi wengine mlipofanya jambo hilo, kwenye karamu yenu ya kimadhehebu, mkijirudisha moja kwa moja katika jambo lile lile ambalo Mungu alilaani tangu mwanzo. Hiyo ni Kweli kabisa. Wakati wo wote ambapo kanisa liliwahi kuwa na ufufuo … Katika wakati wa Luther, ndipo … Ni kitu gani kilichotukia? Wamethodisti … kote kote katika nyakati … Zwingli, Finley, Finney, hao wengine wote, walipokuwa na ufufuo, walifanya nini nao? Waliutupa moja kwa moja katika karamu ya kimadhehebu, na wakatambaa na

kuingia pamoja na hao wengine, wakawabandika chapa kama hao wengine. Ndipo mna kundi la watu linalowatawala. Roho Mtakatifu hawezi kusonga mbele zaidi. Hiyo ni kweli kabisa. Ukianza kuhubiri jambo fulani linalofundishwa na Biblia, unalipenda, na madhehebu hayo hayaliamini; wanakufukuza moja kwa moja. Jaribu mara moja uone kama ni kweli ama si kweli. Mtaona ya kwamba ni Kweli. Mnaona, kwenye karamu ya kimadhehebu kila wanapoitiwa hayo, hiyo karamu ya Balaamu, shida inaingia. Loo, Luther, Wesley, Pentekoste, na hao wote ni wahanga wake.

88 Angalia, hapo ndipo basi, haleluya, wakati Musa alipojitokeza na kusema, "Ni nani aliye upande wangu na wa Mungu?" Amina! Hapo ndipo yule Mlawi alipouchomoa upanga wake na kupitia kambini na kuangamiza kabisa kila kitu kilichokuwa na uhusiano na jambo hilo. Amina! Kila kitu; kila mwanamume aliyekuwa na mwanamke wa Kimoabu, waliwaua papo hapo wote wawili pamoja. Sasa saa imewadia. Yuko wapi huyo mtu? Wako wapi wana wa Haruni, baadhi ya ukuhani ambao wako tayari kulichomoa Neno la Mungu, Upanga huu wenye makali kuwili? Kasema, "Ni nani anayesimama upande wangu na Mungu?" Yuko wapi? Waweza kualika, kualika bali hakuna mtu anayejibu. Mnaona ninalomaanisha? Hatulipati. Tunaninii tu … Kuna kasoro. Angalia, hao hapo … Hapo ndipo Musa aliposimama na kusema mambo haya.

89 Angalia, dhambi yao, waliyotenda kule, walipojiundia madhehebu pamoja na Wamoabu na kuwafanya mwili mmoja… Hiyo dhambi hawakusamehewa kamwe. Nitaenda tu kwenye hilo kwa dakika moja tu. (Tumechelewa, bali hebu kidogo tu.) Hawakusamehewa dhambi zao kamwe. Hakuna hata mmoja wao aliyewahi kuingia katika Nchi ya Ahadi. Yesu alisema, katika … Samahani. Yohana Mtakatifu 6, Yesu alisema; katika Yohana Mtakatifu 6, waliposema, "Baba zetu walikula mana jangwani" … Walikuwa ni Wapentekoste. Ndugu, walikula mana, walikuwa na kitu halisi.

Yesu alisema, "Nao, kila mmoja wao, amekufa. Wameangamia. Wamepotea Milele." Hawakusamehewa dhambi zao kamwe. Walifanya nini? Walivunja agano lao na Mungu, na kujiunga pamoja na Balaamu, yule nabii wa kukodiwa ambaye asingekubali onyo la Mungu; asingechukua Neno la Mungu; asingechukua kitu chochote cha Mungu. Lakini alikuwa ameyakinia kuwaunganisha wote kuwa mmoja. Unaweza kuona huo ujinga? Ningeweza kukaa kwenye jambo hilo kwa muda mrefu, lakini na—nafikiri mmelipata. Mnaona? Angalia, kamwe hawakusamehewa dhambi yao; hakuna hata mmoja wao aliyeishi chini ya baraka hizo na kula hiyo mana na kila kitu.

90 Wakati Ujumbe halisi na wa kweli ulipofikia kwenye shindano la kuamua, waliuundia madhehebu. "Tutawachukua Wamoabu na sisi pamoja. Wao ni madhehebu makubwa, taifa kuu. Sisi hata si… Sisi hata si taifa. Tutaoana tu mmoja kwa mwingine na—na tutakuwa sawa wakati huo. Tutakuwa pamoja nao." Na haikusamehewa kamwe; kamwe, kamwe hawakusamehewa.

Yesu alisema, "Wao, kila mmoja wao, *amekufa*." Hebu tafsiri neno hilo katika Kiebrania ama Kiyunani, mojawapo, ama hata katika Kiingereza, linamaanisha "Utengano wa milele"; wamepotea milele. Hiyo ni kweli.

Loo, naam, waliona miujiza. Waliona Neno limetiwa mafuta. Wanakula mana iliyotoka Mbinguni. Walifurahia baraka za upatanisho. Waliona Mwamba uliopigwa ukitoa maji Yake. Walikunywa Kwake. Waliufahamu Huo kibinafsi. Lakini ilipofikia kuvunja Neno hilo … Usisahau kamwe jambo hilo! Wakati Yesu aliposema, "Mimi na Baba Yangu ni mmoja," hakusema kuna watatu. A-ha? Wakati haya mambo mengine yote makuu ya kimsingi ya Maandiko…

91 Mtu mmoja alinijia hivi majuzi usiku kunionyesha mahali nilipokosea, ama kuzungumza juu ya utatu. Nina maelfu ya marafiki wazuri wa utatu. Wako katika Babeli hiyo. Nina marafiki wengi wa Umoja katika Babeli hiyo, pia. Mnaona? Lakini ni jambo gani lililotukia? Mtu mmoja alisema, "Ni suala la msamiati, Ndugu Branham. Unaamini utatu?"

Nikasema, "Hakika." Nikasema, "Nitachukua neno lako: msamiati." Nikasema, "Unaaminije jambo hilo?"

Akasema, "Ninaamini katika Mungu mmoja."

Ninasema, "Unafanya vizuri." Mnaona?

Akasema, "Ninaamini kuna Mungu mmoja, na nafsi tatu katika Uungu."

Nikasema, "Hivi wewe si mwa—mwanafunzi wa BIOLA?"

Akasema, "Naam."

Nikasema, "Ndivyo inavyosikika." Nikasema, "Hilo halishuhudii mazuri sana kwa elimu uliyo nayo." Nikasema, "Watu watatu, na Mungu mmoja?" Nikasema, "Kulingana na Webster, hapo, haina budi kuwa ni utu kabla ya kuwa mtu. Unaamini katika miungu watatu, bwana." Huwezi kuwa mtu bila kuwa utu, maana inahitaji utu kumfanya mtu.

Kwa hiyo wanasema … Akasema, "Vema, Bw. Branham, unajua, hata wa—wanatheolojia hawawezi

kulielezea hilo."

Nikasema, "Hiyo ni kweli kabisa. Neno halimjii mwanatheolojia." A-ha. Nikasema, "Biblia yote imefungwa katika Ufunuo, 'Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, wala milango ya kuzimu haiwezi kulishinda.'" Mnaona? Amina, haya basi. Mnaona? Lakini basi inapofikia mambo hayo … Loo, jamani!

92 Sasa tunataka kuharakisha na kufunga upesi sana kama tunaweza. Sina budi kupita baadhi ya Maandiko haya na maandishi, mnaona. Sasa, angalia, hawakusamehewa kwa yale waliyofanya. Walifanya nini? Walifurahia baraka. Msisahau jambo hilo. Nitarudia hilo tena. Kamwe hawakusamehewa jambo hilo. Kumbukeni, kanda hii inaenda kote ulimwenguni. Mnaona? Inachezwa katika kambi huko Afrika, India, kote ulimwenguni; inafasiriwa katika lugha mbalimbali; na kambi mbalimbali, sehemu mbalimbali. Dhambi hiyo haikusamehewa kamwe. Nini? Wao …

Unasema, "Vema, Mungu atukuzwe, ni—nilifanya jambo hili. Ni—ni—nimefanya jambo hili. Nimekula mana ya Mbinguni. Mimi …"

Naam, walifanya hivyo, pia. Naye Yesu akasema, "Wao, kila mmoja wao, amekufa." Lakini ilipofikia kwenye Ujumbe halisi, ambapo, hawapaswi kuvunja Agano hilo, na taifa lingine. Mungu alikuwa mbaguzi na Yeye aliwatenga watu hao, nao hawakupaswa kuwa na uhusiano wowote na mtu mwingine yeyote, kumwoa mtu yeyote. Nalo Kanisa halisi, na Bibi-arusi halisi na wa kweli wa Kristo, ameunganishwa na Kristo ambaye ni Neno. Nawe huoi na kuolewa katika shirika lolote, dhehebu lolote. Wewe dumu kabisa na Kristo na Neno hilo, kama mtu binafsi. Kufanya hivyo ni kujitenga Milele na Mungu. Ninatumaini kila mtu analipata hilo.

93 Sasa, katika fungu letu, ilikuwa inakaribia Sikukuu ya Pasaka; ilikuwa ikienda kuadhimishwa. Ulikuwa ni wakati mbaya sana. Watu walikuwa wamelala nje ya malango. Kila pasaka ilifanya jambo hili. Walikuwa nje wamelala chini. Nyumba za wageni zilikuwa zimejaa na kila kitu. Ilikuwa ni pasaka. Kulikuwa na matarajio makubwa mle ndani. Hewa yote ikajazwa. (Sasa, mnamo dakika tano zaidi nitakuwa nimetoka, Bwana akipenda, ama kumi.) Kila mtu alikuwa amehemukwa.

Angalia, kuna tabaka tatu za watu pale. Mnaona, kulikuwako na matarajio makubwa. Walijua ya kwamba mtu huyu wa ajabu alikuwa anakuja kwenye karamu hii. Baadhi yao walimpenda; walimwamini. Baadhi yao *walimchukia*; wengi wao walimchukia. Na kwa sababu mmoja alimpenda na mwingine alimchukia, mtu wa katikati *hakujua* la kufanya. Mnaona? Hawakujua. Angalia, hewa ilikuwa imejaa matarajio. Mmoja akisema, "Atakapofika kule juu, ninakwambia tutamwita… Tutampa jaribio la Neno. Tutamsimamisha kule juu kwa kuhani mkuu. Tutaona hekima Yake ilivyo dhidi ya Kayafa." Alikuwa tayari amethibitisha jambo hilo. Mnaona?

94 "Lakini tutafanya hivi: Tutaona … Ninajua ya kwamba baadhi ya viongozi wakuu watamshika. Jamani, watamshambulia maskini jamaa huyo kwelikweli. Watamfanya ajue alichokuwa, wanapoanza kuchezacheza na makuhani wetu. Jamani, wanajua wanachofanya. Wao ni watu werevu. Wanajua wanachofanya."

Wengine walisema, "Sijui watamfanyia nini jamaa huyo hata hivyo."

Wengine walisema, "Loo, ninamngojea Yeye aje. Mungu yuko pamoja Naye. Yeye ni Neno hilo. Loo, ninataka tu—ninataka tu kumwona." Mnaona? Loo, walikuwa wamegawanyika. Sasa, mnaona, wale waliomjua na kumwamini, wangejua watangoja kwenye lango lipi. Mnaona? Walijua Yeye angekuja kwa njia gani. Kuna matarajio makubwa, lakini mnajua, hakukuwa na wengi sana waliomwona. Mnaona, kuna wengi ambao hawakumwona. Ndivyo ilivyo leo.

95 Baadhi yao walisema, "Yeye ni mtu mzuri. Loo, hakuna kasoro Kwake. Kama Napoleon, Washington, alikuwa mtu mzuri. Lakini, loo, kama mwalimu, la, la."

Baadhi yao walisema, "Loo, Yeye ni mtu mzuri. Loo, Yeye—Yeye amechanganyikiwa kabisa, hivyo tu. Yeye ni jamaa mzuri. Hakuna mtu anayeweza kusema lolote baya juu Yake."

Wengine walisema, "La, Yeye—Yeye ni pepo. Ninaweza kukwambia ya kwamba—ya kwamba upuuzi huo wa kusoma mawazo na upuuzi huu mwingine wote, na huo—huo ni unabii wa uongo. Ni kinyume cha kanuni zetu za imani. Usiamini kitu kama hicho."

Na huyo mwingine, akasema, "Utukufu kwa Mungu, ni Mungu. Ninamjua. Ninaona." Nao walikuwa wakingojea. Sasa hivyo ndivyo tu tunavyosimama leo, bali ni jambo lile lile: Neno lililotiwa mafuta kwa ajili ya wakati huu; wakati wa Kanisa la Laodikia.

96 Sasa tutafunga kwa kusema jambo hili. (Kitambo kidogo tu.) Tabaka tatu zilimngojea. Ndivyo ilivyo leo, hiyo ni kweli, tatu. Angalia, waaminio walikuwa wakipaza sauti. Mnaona? Mnaona? Huduma Yake ilikuwa imemfanya kupendwa na wengine, kuchukiwa na wengine, na tabaka nyingine kumshangaa. Mnaona? Huduma Yake … Hebu ninukuu jambo hilo tena. Huduma Yake, cho chote ilichokuwa … Tunajua

sasa, lilikuwa ni Neno. Lakini *huduma* Yake ilikuwa imewafanya watu fulani wampende. Walichaguliwa tangu zamani kufanya jambo hilo. Mnaona, waliamini jambo hilo. Waliliona. Hakukuwako na zaidi … Wakati Nathanieli alipokuja pale, na—na Yeye akamwambia yale aliyofanya namna *hiyo*, alisema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli, hakuna swali moyoni mwangu."

Simoni alikuwa amesimama pale, akasema, "Loo, Andrea, mimi sitaenda kule. Nimesikia mambo hayo yote hapo kabla."

"Lakini," Andrea, "yakupasa uje. Unapaswa kuja, uje tu pamoja nami wakati mmoja."

Na wakati alipokuwa ameketi pale, Yesu alimwona akija, mwajua, akija. Kasema, "Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona." Hakukuwa na swali tena. Mnaona, ni hayo tu. Walikuwa kule. Waliamini. Waliliona jambo hilo. Walijua hivyo ndivyo Masihi alivyopaswa kufanya wakati atakapokuja.

97 Ilimbidi awe Nabii, kwa kuwa Musa alisema, "Yeye angekuwa ni Nabii." Na hao waliochanganyikiwa walikuwa wameishi miaka mia nne bila nabii. Ilihitaji nabii kulinyoosha, daima katika kila wakati. Na huyu hapa alikuwa amesimama pale.

Hakukuwa na swali kwao. Walikuwa wakingojea pale wakiwa na mitende mkononi mwao, "Atakuja baada ya kitambo kidogo." Wakingojea!

Mji mzima, una wasiwasi. Wakasema, "Hilo ni kundi la washupavu wa dini waliokusanyika huko nje langoni."

Yule mwingine alisema, "Sijui atafanya nini atakapokuja hapa. Mnajua, kweli ni—ninaamini ya kwamba yeye ni wa bandia. Ninaamini ana mguu wa sungura anaosugua nao sikio Lake, mnajua, ama kitu fulani kama hicho, mnajua."

Na kama wanavyosema siku hizi, "Loo, ni namna fulani ya telepathia ya akili. Ni—ni kitu fulani …" Wanaweza kulielezea lote mbali.

Mwingine alisema, "Huyo ni ibilisi. Wewe kaa upande huu wa mji. Usiwe na uhusiano wowote na jambo hilo. Usishirikiane katika mkutano huo. Usishuke uende kule, mnaona. Hatutakuwa na uhusiano wowote nalo." Tabaka tatu za watu.

98 Sasa angalia. Sasa huyu hapa anakuja amepanda mjini. Vile vile hasa Neno lilivyosema angefanya. Akipanda punda mdogo, akija mjini. Wale ambao hawakuwa wakiangalia kanuni ya imani, hawakuangalia Hekalu, hawakuangalia mambo haya mengine yote, hawakuwaangalia makuhani, yale waliyosema. Wale waliomwamini, walikuwa wamesimama pale wakiwa na mitende mkononi mwao. Wakingojea tu hatua ya kwanza. Hujawahi kuwasikia wakisema, "Ni nani huyu anayekuja?" Loo, la! Walijua ni Nani aliyekuwa akija. Wanajua kile Neno lilichosema. Mnaona? Na hao tabaka nyingine, mnawaona wamerudi mjini? Na ndipo waliposikia kelele hii: "Hosana kwa Mfalme! Hosana kwa Mfalme ajaye katika Jina la Bwana. Hosana! Hosana!" Na makelele yote!

Makuhani walitoka mbio wakaone mchafuko huu wa kidini ulikuwa ni wa nini. Nao watu wakasema, "Ni nani huyu?" Walikuwa wapi kule, marafiki? Sikukuu ya kidini! Mungu yule yule aliyekuwa nao kuadhimisha Sikukuu hii, aliwaambia ya kwamba angekuwa pale namna hiyo tu, nao wakalia, "Ni nani?"

99 Wakati haujabadilika. Watu wameumbwa kama vile walivyokuwa wakati huo. Waebrania 13:8 ilisema, "Ni yeye yule jana, leo na hata milele." Sasa nitafunga kwa kusema hivi: Swali si kwao tena. Waliuliza, "Ni nani huyu?" Lakini katika mwaka wa 1964, swali ni: "Mnasema ni nani?" Haya yote yanahusu nini? Mmesimama kuyachunguza Maandiko? Unafikiri Huyu ni nani? Ni telepathia ya akili? Je! ni kitu fulani cha wenda wazimu kutoka huko jangwani mahali fulani, kama walivyosema, "Yohana alikuwa ni mtu, mshenzi, aliyekuwa akiwazamisha watu huko majini." Wakati, Isaya alisema angekuwa pale, mtangulizi. Malaki ilisema angekuja vivyo hivyo hasa. Hao manabii walisema, "Nabii huyu atatoka moja kwa moja kule kutangulia jambo hilo." Naye alikuwa hapa.

Wao walisema, "Huyo ni mshenzi. Kaa mbali naye. Mnaona? Usiwe na uhusiano wo wote naye." Na huyu hapa Masihi anakuja, vile vile hasa Maandiko yalivyosema, "Ya kwamba atapanda mjini juu ya mtoto wa punda. Mpole na mnyenyekevu, amepanda mwana punda, akiingia mjini, Maandiko yapate kutimizwa." Na hawa hapa watu wamesimama kwenye sikukuu ya kidini tena, kama Balaamu, kwenye sikukuu ya kidini, wakisema, "Ni nani Huyu?"

Na siku hizi, Maandiko yaliyoahindiwa kwa ajili ya wakati huu, wapendwa, yametimizwa moja kwa moja katikati yetu, saa baada ya saa. Mnafikiri ni nani? Na tujifunze juu Yake tunapoinamisha vichwa vyetu.

100 Mungu mpendwa, sote tunafikiria kwa makini, kwa kina, kwa sababu hatuna budi kufanya jambo hili. Liko mikononi mwetu, Bwana. Tunakuona Wewe, Mfalme mkuu. Tunaona ahadi Yako ya Neno. Tumekuwa tukitazamia jambo hili kwa miaka mingi, kwa ajili ya wakati huu mkuu ujao, wakati tunaishi sasa hivi.

Tunaona Neno Lako lililotiwa mafuta katika watu Wako, wakiliishi, vile vile hasa ulivyosema lingetukia. Tunaona kundi la Shetani limetiwa mafuta huko ng'ambo. Nasi tumelifananisha na taifa lote, huku na huko kupitia Neno, kwa hiyo hakutakuwako na jiwe hata moja litakalosalia bila kufunuliwa. Sijui ni nani uliyemkusudia uzima, Bwana. Si kazi yangu kujua jambo hilo, hiyo ni kazi Yako. Lakini ni kazi yangu kusogeza kila jiwe. Mungu na anisaidie, awasaidie watu wengine wanaoamini jambo hilo. Fanya kila linalowezekana, Bwana, kusudi kusiweko na yeyote uliyemchagua ila ambaye atasikia hilo.

Tunataka kuona kuja Kwako, moja kwa moja katika kizazi chetu, Bwana. Tunaamini jambo hilo. Tunaamini ya kwamba—ya kwamba kuna Ijumaa nyingine ya Mtende; Ijumaa Kuu na Ijumaa ya Mtende. Kusulibishwa kwa Kanisa Lako, bali ushindi wetu utakapokuja umepanda mwana punda.

101 Tunaomba, Mungu, ya kwamba utabariki, leo, watu Wako. Bariki kanisa hili dogo. Mbariki mchungaji huyu mpendwa na mwanawe hapa, Ndugu Outlaw na—na mwanawe; wote wawili Jimmy Sr. na Jr. Mbariki kila mtu aliye humu ndani.

Mungu, jalia kamwe tusije hapa asubuhi ya leo … Naomba … Kamwe sikusafiri kutoka Tucson kuja tu … Kama ningekuwa na majaliwa ya kuzungumza na watu fulani, Bwana, ha—haikuwa ni—kutukuza kitu ila Mtu huyu, ambaye watu wanashangaa ni nani. Wanajua ya kwamba mwanadamu hawezi kufanya jambo hili. Wanajua inapita uwezo wa mwanadamu kujua mambo haya. Lakini watu wanasema, "Ni kitu gani?"

Bwana, tunajua ni Wewe. Ni Yesu Kristo, katika utu wa Roho Mtakatifu. Yeye ni Roho Mtakatifu. "Nimetoka kwa Mungu. Ninaenda kwa Mungu." Nasi tunaona ile Nguzo kuu ya Moto miongoni mwetu, Bwana. Ni kama walivyofanya katika sehemu ya kwanza ya Biblia pamoja na Musa. Tuliiona katikati ya Biblia wakati Paulo alipokuwa akienda zake Dameski. Tunaiona. Sasa hapa tunaiona katika wakati wa mwisho tena. Tatu ni thibitisho. Imekuwa ni Ujumbe kila wakati.

Mungu, jalia wanaume na wanawake wasishikilie tena mapokeo na kanuni za imani. Lakini jalia watoke kwenye kitu hicho, wampe Mungu maisha yao kabisa na waamini; si kutegemea nadharia tu na mambo ya mwanadamu, bali kumtumainia Mungu aliye Hai. Wakati sikukuu hizi zinaendelea, kilio bado ni: "Ni nani huyu? Ni kitu gani? Inahusu nini?" Watu wa dini wanasema jambo lile lile. Na ni Bwana Yesu yule yule, aliyefanyika mwili katika watu Wake, akilitia mafuta Neno Lake kwa ajili ya Bibi-arusi. Nao hawawezi kufahamu jambo Hilo. Wote wamemezwa kabisa katika Laodikia, mpaka hawajui hayo yote ni kitu gani. Lakini nabii alisema, "Kutakuwako na Nuru jioni." Kwa hiyo sasa, tunamtazamia, Bwana. Njoo, Bwana, mbariki kila mmoja.

102 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa, na mioyo yenu. Unaamini jambo hili kuwa ni Kweli? Unaamini? Inua tu mkono wako, useme, "Kwa kweli ninaamini jambo hilo kuwa ni Kweli, ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Tupo hapa sasa na ninaamini tumechanganyikiwa sana…" Ulikuwa mkutanoni juzijuzi, wakati ngano, shina … Mnaona, hatukuwa na madhehebu ya kufuata jambo hili. Nimekuwa papa hapa pamoja na mchungaji wenu wakati wote, mwaka rudi mwaka nenda. Kwa kawaida, miaka miwili ama mitatu na unaeundiwa madhehebu. Haukuunda madhehebu wakati huu. Hauwezi. Kapi likajiondoa Kwake, bali hakuna maendeleo ya zaidi. Ngano, huduma imegeuka moja kwa moja ikarudi jinsi ilivyokuwa pale mwanzo. Ni Yesu Kristo miongoni mwetu, rafiki. Si mtu fulani, ila yule Mtu Kristo Yesu anayeishi ndani yako, naye anataka kuwa sehemu ndani yako, nawe uwe sehemu Yake. Hivi hutampokea leo?

103 Kuna yeyote hapa ambaye hajapokea ubatizo wa Roho, bado? Sasa unasema, "Ndugu Branham, nakwambia, nilipaza sauti wakati mmoja." Hilo ni zuri sana. "Nilinena kwa lugha wakati mmoja." Hilo ni zuri sana, pia. Lakini bado hilo silo ninalozungumzia. Unawezaje kupaza sauti na kunena kwa lugha na kulikana Neno? Ushahidi wa Roho Mtakatifu ni kuamini Neno Lake. Daima imekuwa hivyo katika kila wakati kama unaweza kulipokea Neno. Wale makuhani walikuwa wamemzidi Yesu kwa maili milioni moja inapofikia kwenye matunda ya Roho: wenye utu wema, na wenye amani, na wapole, na wanyenyekevu. Aliyararua makanisa, akawatoa nje; na kuwachambua watu, na kuwaita "wadanganyifu" na kila kitu. Mnaona? Lakini Yeye alikuwa ndiye hilo Neno. Yeye alikuwa Neno hilo. Hivyo ndivyo ilivyo: mwamini Mungu. Mungu ni Neno. Liamini.

104 Kama kamwe hujapata kupokea ubatizo wa Kikristo bado, kuna kidimbwi hapa. Kamwe hujampokea Roho Mtakatifu halisi bado, ambaye anakufanya ujue ya kwamba kila Neno la Mungu ni Kweli; unasema, "amina" Kwa Neno Hilo na unaliamini kwa moyo wako wote, basi unaweza kumpokea asubuhi ya leo. Na ndipo hutashangaa kwamba Huyu ni nani anayewafanya watu watende jinsi wanavyotenda. Utajua ni kitu gani. Kama huna tukio hilo, ungesema, "Ndugu Branham, nikumbuke katika maombi yako, nami nitainua mkono wangu"? Nawe unasema, "Nami nita—nita- …" Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, wewe. Mungu akubariki, hilo ni sawa. Mungu akubariki, vema.

105 Ee Mungu, muziki mtamu unapocheza vizuri … Loo, Yeye ni wa ajabu! Hakika. "Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa milele." Ninaomba ya kwamba utawapa watu hawa, Bwana. Ninaweza tu kuomba. Hilo tu ndilo ninalojua kufanya, ni kuwaombea. Waliinua mikono yao. Ninafanya kama nilivyowaahidi kufanya, ninaomba ya kwamba utawapa tukio hili kuu; sio tu mhemuko wa hali fulani,

bali tukio la kweli; kukutana na Mungu kama Musa alivyofanya huko kwenye ardhi ile akiwa katika Utukufu wa Shekina; na si pale tu, bali wasiliache Neno hilo kamwe, waende moja kwa moja mpaka waingie kwenye Nchi ya Ahadi Nalo. Mungu, mjalie kila mmoja, asubuhi ya leo.

Kuna magonjwa miongoni mwetu leo, Mungu. Tunaomba ya kwamba utaponya hilo. Mponye kila mgonjwa, kila mhitaji. Jalia, Bwana. Wao ni Wako sasa. Ninawakabidhi Kwako katika Jina la Yesu. Amina.

106 Ninasikitika, nimetumia hapa saa mbili kamili. Lakini angalia, mna jioni yote. Mnaweza kwenda nyumbani na kupata nguvu tena na kulala kidogo. Lakini msisahau yale niliyowaambia. Nimewaambia kutoka moyoni mwangu. Ninajua linasikika jambo la ajabu. Miaka michache iliyopita nilikuja hapa Phoenix pamoja nanyi watu, nikiwaponya wagonjwa kwa maombi ya imani. Kamwe sikulielezea, sikutaka kulielezea. Niliangalia tu nione vile watu wangefanya, nikaangalia tu uigaji na mambo mengine yakiinuka. Limekuwa ni jambo kubwa kwangu kuangalia.

Lakini sasa, ninakuja kwenu na Ujumbe ambao ishara hiyo ilithibitisha. Kanisa lilifanya nini … La, halikuunda madhehebu kamwe. Lakini ni nini kilichowapata madhehebu juu ya uamsho huu? Walifanya nini? Walienda moja kwa moja mpaka Laodikia. Mamilioni na mamilioni, na mabilioni ya dola yalimwagwa katika huo, na ninii tu…nalo limekuwa kubwa na tajiri na linajenga majengo yanayogharimu mamilioni ya dola na vitu kama hivyo. Na kupokea Ujumbe? Hakuna hakika. Wanalikataa. Ni kitu gani? Kapi limejiondosha kwenye ngano. Sasa ngano haina budi kuwa hivyo, ikae katika Uwepo wa Mwana ipate kuwa Injili kamili, punje iliyoiva vizuri kabisa kwa ajili ya Bwana. Hutaliamini? Huyu ni Nani, hata hivyo? Ni Nani? Inaweza kuwa ni mwanadamu? Inaweza kuwa ni kanisa? Inaweza kuwa ni madhehebu? Ni Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Je! Mnamwamini?

107 Sijui sasa, hebu tuabudu kidogo baada ya Ujumbe unaokatakata namna hiyo,… Dada, vipi kuhusu kutupa sa—sa—sauti, pamoja na kwaya hii ndogo hapa, juu ya *Nampenda*. Mnajua ule wimbo wa kale?

Nampenda, nampenda
Sababu alinipenda kwanza,
Akanunua wokovu wangu
Katika Kalvari baridi, yenye giza.

Mtauimba pamoja nami? Ninyi nyote sasa, katika kuabudu tu. A—abudu tu pamoja nami.

Nampenda, …

Sasa, kumbukeni, kama televisheni, Yeye yuko chumbani mwako.

Sababu Yeye alinipenda
Akanunua wokovu wangu
Mtini pa Kalvari.

Je! Mnatambua hilo lilimaanisha nini? Mnaweza? Je! mnapata kilindi chake, yale aliyofanya?

Nampenda, …

Simwoni, bali Yeye yuko hapa. Nina chombo kidogo cha kupokelea hapa ndani, kitu kidogo ambacho kinawaka moyoni mwangu. Ninajua kinamwakisi Yeye. Yeye yuko hapa.

… alinipenda
Akanunua wokovu wangu
Mtini pa Kalvari.

108 Sasa, ninawatakeni mfanye jambo hili, tunapoimba. Sasa tumechanganyikana inapofikia kwenye kile tulichokuwa. Kumbukeni, asili yangu ilikuwa ni ya Kikatoliki. Mnaona? Sasa sisi sote tumechanganyikana hapa, bali tumetoka kwenye upuuzi huo wote sasa. Sisi ni mali ya Kristo. Sisi ni Wake. Sasa wakati tunapouimba huu, hebu na tugeuke tu na kupeana tu mikono. Si lazima usimame. Sema tu, "Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, dada," tunapofanya hivyo, katika mazingira halisi ya Kikristo. Ninaamini Mungu anapenda kuabudiwa. Hivi hamwoni hivyo? Mwabuduni. Yeye … Mungu ni kitu cha kuabudiwa. Nasi tunataka kumwabudu. Na tunafanyaje …? Mnapendana. Mnataka kutendeana mmoja kwa mwingine… "Kadri mnavyowatendea hawa, mtanitendea Mimi."

Hebu na tuuimbe sasa, na—na kupeana mikono, na kuabudu pamoja …

… kwani Yeye …

Mungu akubariki.

Loo, ninampenda, ninampenda
Sababu Yeye alinipenda kwanza
Akanunua wokovu wangu
kwa …

Sijui, je, hilo linauchoma moyo wako? Je! Kuna kitu fulani mle ndani ambacho kina—kinajisikia vizuri sana? Unajua, unajisikia kama kwamba ungetaka tu kukitoa hapa nje na kukikumbatia. A-ha? Unajisikia hivyo moyoni mwako? Kama hujisikii, ewe rafiki, kuwa mwangalifu. Uko mahali pa hatari, unaona, kama

hakuna upendo halisi mle ndani, kitu fulani, "Ninampenda." Si wimbo tu, bali ukweli. Alinipenda kwanza. Ningekuwa wapi, leo … Nina umri wa miaka hamsini na mitano. Maisha yangu hivi karibuni yatakwisha. Mnaona? Na kile mimi … Akanunua wokovu wangu … Ndugu Trow, ungeweza nini …? [Ndugu fulani anazungumza kutoka kwa kusanyiko — Mh.]

109 Mlisikia ushuhuda huo, "Kuokolewa."

Nimeokolewa kwa nguvu Zake za Kiungu,
Nimeokolewa kufikia kwenye kipeo kipya cha utukufu!
Maisha sasa ni matamu furaha yangu imekamilika,
Kwa kuwa nimeokoka!

Unajuaje? Roho yangu inashuhudia pamoja na Neno Lake ya kwamba nimepita kutoka mautini nikaingia Uzimani.

Asanteni, Wakristo wapendwa. Hilo linanifurahisha. Ninapenda kuja mahali kama hapa ambapo unajisikia uko nyumbani. Ni vigumu kwangu kuondoka. Ninaendelea tu kuwazia, kuangalia ile saa ya ukutani; na—nami ninamwona binti yangu ameketi pale, akinitikisia kichwa chake, na akiangalia chini namna hiyo; na—na mwanangu, ameketi hapa juu, akisema, "Kwa nini—kwa nini unawachelewesha hapa?" Sijui. Ninataka tu kuketi huku … mnajua. Sijui. Ninapenda ushirika. Mnajua, siupati mahali pengi sana (mwajua jambo hilo), panapungua sikuzote. Lakini ninajua ninakaribia kule. Mnaona? Na siku moja nitahubiri mahubiri yangu ya mwisho, kuifunga Biblia mara ya mwisho. Nitasafiri kidogo basi. Njoni mkanitembelee nitakapoondoka. Njoni, nasi tutaketi tu chini milele, na kuzungumza kama Ndugu Carl alivyosema, na kuishi milele.

110 Sasa angalieni, marafiki, nitawaulizeni jambo ninalowataka mfanye. Sasa nimekuzuia usipate chakula chako cha jioni. Mnaona? Na sasa, Ndugu Outlaw alifanya jambo fulani muda mfupi uliopita … Yeye mara chache sana hufanya jambo lolote nisilopenda. Lakini—yeye alichukua sadaka kwa ajili yangu, mnaona. Sijui kama mmoja wao atarudi, na kurudisha matoleo hayo huko nyuma, na kusimama mlangoni. Nawe nenda ukaichukue na ununue chakula chako cha jioni nayo. Hiyo ni zawadi kutoka kwangu, kurudi kwenu. Mnaona? Fanyeni hivyo. Mnaona? Hilo litakuwa sawa. Yeye ni mtu mzuri. Yeye daima … Yeye kamwe … Mimi kamwe siendi mahali po pote wala cho chote kile bila yeye—yeye hutaka kunifanyia jambo fulani la kunisaidia. Hiyo ndiyo njia yake.

111 Kuna mtu fulani anayesimama hapa; Ni—ninaogopa kuyataja majina yao, huenda ikawaudhi. Kuna ndugu wa thamani ambaye ameenda tu Utukufuni, ameenda upesi. Shauku Yake … Alijua nilipenda msituni, kwa hiyo alitaka kunininulia gari aina ya jeep. Nisingemruhusu afanye hivyo. Ndipo baada ya yeye kuondoka, mke wake mdogo alitaka kufanya jambo hilo, nami nisingemruhusu kufanya hivyo. Lakini wale wavulana wengine walikusanyika pamoja wakaenda hapa … Na—na kuna ndugu mwingine anayekuja kwenye kanisa hili, kasema, "Ndugu Branham, ninaunda magari ya mchanga." Mnajua, vigari vya farasi; ama mnavyoita *hacks*. Kisha akasema, "Nitakutengenezea moja ya hayo." Nisingemruhusu. Mnajua walichofanya hawa wavulana? Walitengeneza gari aina ya jipu na tela ya mchanga pamoja. Sijawahi kuona moja kama hilo.

112 Kutoka kwenye mkutano wa Tucson usiku huo, waliileta kwenye ua langu, na kusema, "Hii ni zawadi kutoka kwa watu wa—wa Phoenix." Mnaona, hata wasingejihesabu wenyewe tu, walisema tu, "Loo, ni sisi sote pamoja, mnaona." Hiyo ni … Loo, ni—ninajua tu kama ninaweza kamwe kwenda Mbinguni, nitaishi na watu kama hao. Hilo lilimaanisha mengi sana kwangu, mwajua, kitu kama hicho tu; haya madogo … kitu fulani.

Hilo linanifanya kujisikia hivyo kwa Ndugu Outlaw hapa. Sema, "Vema, Ndugu Branham, ninaninii tu …" Kwenda mahali fulani hapa kwa baadhi ya…unakwenda tu mahali fulani mpaka wanaanza kukupenda wewe, na kuzungumza na wewe, na kuzungumza habari za Yesu. Na—na watu wa … Vema, unajua, "Ndege wa manyoya." Mnajua, wanapenda kukusanyika pamoja na kuzungumza juu ya mambo, kushirikiana pamoja.

113 Nami ni—ninathamini jambo hilo, bali si—sikutaka matoleo, ndugu, dada. Mimi…kanisa langu hunipa mshahara mdogo wa dola mia moja kwa juma na huo unanitosha. Kwa hiyo ni—ninathamini jambo hilo. Sasa kama ye yote wenu anataka kula chakula chake cha jioni, vema, mtu fulani atakuwa huko mlangoni na mpate chakula chenu cha jioni kutoka kwangu. Mnaona, itakuwa sawa tu. Baadhi yenu, nimewaweka mbali na chakula chenu cha jioni. Mnampenda? Ndipo huna budi kunipenda maana mimi ni sehemu Yake. Mnaona? Amina. Hiyo ndiyo sababu ninawapenda. Bwana awabariki.

114 Hebu na tusimame sasa. Msisahau mikutano yetu ijayo. Wakati wo wote mkiwa karibu, kumbukeni tu, ingia. Daima mnakaribishwa. Mtaniombea? Mimi—mimi ndiye mtu anayehitaji maombi. Mtaniombea? Ni wangapi wanaoweza kutambua uzito huo, yale ninayopaswa kufanya, na mambo yaliyo mbele yangu? Na ninajua yanayokuja, moja kwa moja huko mbele. Mnaona? Ninaweza kuona jambo hilo kama tu vile ninavyoona mambo mengine yakija. Ninajua kinachokuja. Mnaona? Lakini hakuna wakati wa kuzungumza juu ya jambo hilo. Hebu tuzungumze juu ya kile kinachoendelea sasa hivi. Kesho itajishughulisha

yenyewe. Mnaona? Je! Wewe … utaniombea? Sasa, je! mliinua mikono yenu mtaniombea? Vema.

Mungu awabariki sasa. Nitairudisha ibada kwa mchungaji wenu mzuri, Ndugu Jimmy Outlaw. Mungu akubariki, Ndugu Jim.

MESSAGE hub online

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7